# MATUMIZI YA ISTIARI, TASHBIHA NA TAASHIRA KATIKA DIWANI YA SAUTI *YA DHIKI*

**NA**

**MARGARET WANJIRU KARANJA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**OKTOBA 2014**

# IKIRARI

TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA YA AINA YOYOTE KATIKA CHUO CHOCHOTE KINGINE.

……………………………………………..                TAREHE …………………………

MARGARET WANJIRU KARANJA

(MTAHINIWA)

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WALIOTEULIWA NA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

………………………………………………                TAREHE …………………………

PROF. KINEENE WA MUTISO

………………………………………………                TAREHE …………………………

PROF. RAYYA TIMAMMY

## TABARUKU

Kwa mamangu Mary kwa kunipigania nipate elimu. Pia kwa wanangu Wesley na Abishag kwa kunipa changamoto na ari ya kusoma.

## SHUKRANI

Utafiti huu si mchango wa mtu mmoja. Wengi walinishika mkono ili nifaulu. Hivyo sina budi kuwashukuru.

Kwanza namshukuru Mola kwa kunipa uwezo wa kushughulikia kazi hii. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Prof. Kineene wa Mutiso kwa ushauri na kuwa mhimili katika safari ya uandishi wa tasnifu hii. Mola awabariki.

Ningependa kuwashukuru wahadhiri wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika ambao walinipa maarifa ashirafu. Hawa ni Prof. Habwe, Dkt. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Bw. Mungania B.G, Dkt. Mbuthia na Dkt. Iribe Mwangi. Kwao Mungu awazidishie maarifa na busara.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao tuliabiri dau la masomo pamoja hadi ufuoni. Nao ni Margaret Muthoni, Regina Gitau, Sister Teresia, Vincent Oiro, Zsuma, Mariam Ngome, Beatrice Kisakwa, Furaha, Scholar Waweru, Grace Njenga, Julius Mwangi, Magdalene Mulwa na Jael Akinyi. Asanteni kwa kunifaa katika mijadala na kwa ushauri. Nawaombea ufanisi katika kila hali maishani.

Sina budi kumshukuru mamangu Mary Waithira kwa kuhakikisha nimepata mwanga wa elimu na kunitia moyo daima nisonge mbele. Pia wanangu Wesley Mbugua na Abishag Muhito kwa changamoto zenu na ari ili nisome. Vile vile kwa uvumilivu wenu usiomithilika, Mola awabariki.

Labda sikuweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema asante sana.

## KIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **K.H.J** | Kama hapo Juu |
| **U.O.N** | University of Nairobi |
| **KANU** | Kenya African National Union |
| **KADU** | Kenya African Democratic Union |
| **N.K** | Na kadhalika |
| UK. | Ukurasa |

# IKISIRI

Katika tasnifu hii tumeonyesha matumizi ya tamathali tatu za ulinganisho ambazo ni istiari, tashbiha na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* iliyoandikwa na Abdilatif Abdalla (1973). Utafiti umeonyesha kwamba Abdilatif alitumia tamathali hizi tatu kati ya zingine ambazo hazijashughulikiwa katika utafiti kufikia dhamira yake kwa hadhira yake teule. Ni mashairi ishirini tu tumeshughulikia ambayo tulichagua kwa kutumia sampuli ya kusudi.

Katika utafiti huu, nadharia ya uhakiki wa mtindo imetumika ambapo baadhi ya vigezo vyake vimehusika. Nadharia hii iliwezesha kuhakiki viashiria vilivyotumika kuunda tamathali za semi; istiari, tashbiha na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* na kuvipa maana viashiria hivi. Matokeo ya utafiti ni kuwa mwandishi alitumia tamathali za semi; istiari, tashbiha na taashira kwa njia ya kufana na kufikia dhamira yake ya kuficha ujumbe ili usifikie wasiolengwa, kuleta tafsida, kujenga mshikamano wa kisemantiki, kufikia umbuji wa mashairi pamoja na kuboresha kazi yake.Tasnifu hii imeleta uelewa zaidi ya tamathali hizi.

## YALIYOMO

IKIRARI ..................................................... ii

TABARUKU ..................................................... iii

SHUKRANI ..................................................... iv

KIFUPISHO ..................................................... vi

IKISIRI ..................................................... vii

YALIYOMO ..................................................... viii

**SURA YA KWANZA ..................................................... 1**

1.0 UTANGULIZI ..................................................... 1

1.1 Tatizo la Utafiti ..................................................... 1

1.2 Madhumuni ya Utafiti ..................................................... 2

1.3 Nadharia Tete ..................................................... 2

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ..................................................... 3

1.5 Upeo na Mipaka ..................................................... 3

1.6.0 Msingi wa Nadharia ..................................................... 3

1.6.1 Lugha ya Kitamathali na Mtindo ..................................................... 5

1.6.2 Uteuzi na Mtindo. ..................................................... 6

1.6.3 Sarufi na Mtindo. ..................................................... 7

1.6.4 Usimulizi na Mtindo ..................................................... 7

1.6.5 Uchimuzi na Mtindo ..................................................... 8

1.6.6 Mtazamo, Itikadi na Mtindo. ..................................................... 8

1.6.7 Mazungumzo na Mbinu za Uwasilishaji wa Mawazo ..................................................... 9

1.6.8 Muwala na Mshikamano ..................................................... 9

1.7 Yalioandikwa kuhusu somo kwa jumla ..................................................... 10

1.7.1 Istiari, Tashbiha na Taashira kwa jumla ..........10
1.7.1.1 Istiari..........10
1.7.1.2 Tashbiha ..........11
1.7.1.3 Taashira ..........13
1.7.2 Yaliyosemwa kuhusu somo katika kazi mbalimbali ..........16
1.7.3 Yaliyosemwa kuhusu somo katika Sauti ya Dhiki ..........22
1.8 Njia za Utafiti..........26
1.9 Hitimisho ..........27
**SURA YA PILI..........28**
2.0 MSINGI WA KINADHARIA WA TAASHIRA, ISTIARI NA TASHBIHA..........28
2.1 Dhana ya Taashira..........28
2.1.0 Aina maalum za taashira ..........29
2.1.1 Sinekidoki..........29
2.1.2Taniaba ..........30
2.1.3Lakabu..........30
2.2 Mbinu ya Istiari..........30
2.2.0 Aina ya istiari ..........32
2.2.1 Istiari Chakavu..........32
2.2.2 Istiari kuu..........33
2.2.3 Istiari ya kikaida ..........33
2.2.4 Istiari hisimseto..........33
2.2.5 Istiari Sahili ..........34
2.2.6 Istiari radidifu..........34

2.2.7 Istiari mseto ........................................................................................................34
2.2.8 Istiari changamano..........................................................................................35
2.2.9 Istiari ya dhana...............................................................................................35
2.3 Aina za Tashbiha ...................................................................................................35
2.3.0 Tashbiha wazi ..................................................................................................35
2.3.1 Tashbiha fiche ..................................................................................................36
2.3.2 Tashbiha ya Kiutendi ......................................................................................36
2.4 Hitimisho ..................................................................................................................37
**SURA YA TATU ..........................................................................................................38**
3.0 Matumizi ya Istiari, Tashbiha na Taashira Katika Sauti ya Dhiki ..........................38
3.1.0 ISTIARI ............................................................................................................38
3.1.1 N'shishiyelo ni Lilo ..........................................................................................38
3.1.2 Jipu ....................................................................................................................39
3.1.3 Mamba ..............................................................................................................40
3.1.4 Ukamilifu wa Mja .............................................................................................41
3.1.5 Mnazi: Vuta n'kuvute .......................................................................................44
3.1.6 Telezi .................................................................................................................46
3.1.7 Semeni Wenye Kusema ....................................................................................48
3.1.8 Muwerevu Hajinyowi .......................................................................................49
3.1.9 Ah! Mwenzangu ................................................................................................50
3.1.10 Mamaetu Afrika ..............................................................................................51
3.1.11 Jana na Leo na Kesho. .....................................................................................53
3.1.12 Usiniuwe ..........................................................................................................54

3.1.13 Mambo Yana Mambo Yake ..... 56
3.1.14 Watiliye Pamba ..... 56
3.1.15 Wasafiri Tuamkeni ..... 56
3.1.16 La Mjini na La Shamba ..... 58
3.1.17 Ndiya Panda ..... 58
3.1.18 Kichu Hakiwi ni Uchu ..... 59
3.1.19 Zindukani ..... 59
3.2.0 TAASHIRA ..... 60
3.2.1 Jipu ..... 60
3.2.2 Mnazi: Vuta N' Kuvute ..... 60
3.2.3 Telezi ..... 60
3.2.4 Mamaetu Afrika ..... 61
3.2.5 Usiniuwe! ..... 61
3.2.6 Mambo Yana Mambo Yake ..... 63
3.2.7 Watiliye Pamba ..... 63
3.2.8 Wasafiri Tuamkeni ..... 63
3.2.9 Ndiya Panda ..... 63
3.2.10 Kichu Hakiwi ni Uchu ..... 64
3.2.11 Zindukani ..... 64
3.3.0 TASHBIHA ..... 65
3.3.1 N'shishiyelo ni lilo ..... 65
3.3.2 Jipu ..... 65
3.3.3 Siwati ..... 67

3.3.4 Mamba ........................................................................................................67
3.3.5 Mnazi: Vuta N'kuvute ........................................................................................68
3.3.6 Telezi ........................................................................................................69
3.3.7 Semeni Wenye Kusema ........................................................................................70
3.3.8 Muwerevu Hajinyowi ........................................................................................71
3.3.9 Mambo Yana Mambo Yake ........................................................................................71
3.3.10 Jana na Leo na Kesho ........................................................................................73
3.3.11 Usiniuwe ........................................................................................................73
3.3.12 Ndiya Panda ........................................................................................................73
3.3.13 Kichu Hakiwi ni Uchu ........................................................................................74
3.3.14 Zindukani ........................................................................................................75
3.3.15 Hitimisho ........................................................................................................75
**SURA YA NNE ........................................................................................................77**
4.0 Majukumu ya Istiara, Tashbiha na Taashira katika Uwasihishaji wa Dhamira Katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki.* ........................................................................................................77
4.1 Utangulizi ........................................................................................................77
4.2 Majukumu na Dhamira ........................................................................................................77
4.3 Hitimisho ........................................................................................................81
**SURA YA TANO ........................................................................................................82**
5.0 Hitimisho na Mapendekezo ........................................................................................................82
5.1 Utangulizi ........................................................................................................82
5.1.0 Hitimisho ........................................................................................................82
5.1.1 Madhumuni ya utafiti ........................................................................................................83

5.1.2 Matokeo kuhusu nadharia tete ........................................................................83

5.2 Mapendekezo ........................................................................................................83

MAREJELEO ...........................................................................................................85

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Taashira, tashbiha na istiari ni mbinu za tamathali za usemi ambazo hutumika katika kazi za kifasihi kuunda taswira mbalimbali katika kazi hizi. Aina mojawapo ya kazi hizi ni ushairi. Mbinu hizi tatu kama nyinginezo huwa na majukumu matatu katika kazi ya fasihi kulingana na Wamitila (2008) ambaye aeleza majukumu haya kama urembeshaji wa kinachozungumziwa ili kiwe na mvuto mkubwa kisanaa; ufafanuaji wa kinachohusishwa na mwishowe kufanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani. Mbinu hizi zimetumika katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* kufafanua, kufanya imara na vilevile kurembesha kinachorejelewa na lugha kwa jumla.

Tamathali hizi husaidia kuleta hisia za ndani alizonazo mwandishi. Tamathali za semi husaidia kupanga mawazo kwa njia ya mvuto. Hili huleta kufasiriwa kwa uangalifu kwa yale yaliyosemwa. Vile vile huleta ulinganifu unaotoa uzito wa lugha yenye mashiko na iliyoteuliwa. Abdulaziz (1979) asema mshairi ambaye ni mkwasi katika utunzi wa mashairi atarajiwa kuonyesha ufahamu wake wa hali ya juu wa lugha, kufinyanga na kuunda maneno kivyake na kubuni au kuunda mafumbo na mbinu za fasihi katika kazi yake.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Tunachunguza matumizi ya taashira, istiari na tashbihi katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Tamathali hizi za semi zimepewa nafasi muhimu katika jamii nyingi ambapo mashairi au fasihi kwa jumla hukaririwa au kuandikwa. Lugwiri (2011) asema tangu enzi za Aristotle na Plato, tamathali za semi zimetumika kueleza dhana mbalimbali katika jamii. Aidha hutumika kufumbata ujumbe fulani kufikia hadhira teule.

Lugha ya kitamathali kama asemavyo Wamitila (2008) ina majukumu ya urembeshaji wa kinachozungumzwa au kurejelewa na hiyo lugha. Pili, ufafanuaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum. Mwisho huwa na jukumu la uthibitishaji wa kinachorejelewa. Kazi yoyote ya fasihi ambayo kwayo tamathali za semi zimetumika vizuri huvutia hadhira mno kwa urembo wake. Pia huonyesha ubunifu wa hali ya juu na uasilia katika kazi ya fasihi. Wakati mwingine huonyesha mazingira ya mshairi. Kazi ile ambayo haijatumia tamathali za semi vizuri huchosha kwa kukosa mvuto. Kutokana na hayo yote tukachagua kushughulikia matumizi ya tamathali, taashira, istiari na tashbiha katika diwani ya S*auti ya Dhiki*. Tamathali hizi ni baadhi tu ya tamathali nyingine zinazopewa nafasi katika uhakiki wa kimtindo katika uhakiki wa kazi za fasihi.

### 1.2 Madhumuni ya Utafiti

i. Kuonyesha taashira, istiari na tashbiha zilizotumika katika *Sauti ya Dhiki*.

ii. Kutahimini mchango wake katika kuwasilisha dhamira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki.*

### 1.3 Nadharia Tete

i. Mtunzi wa diwani ya *Sauti ya Dhiki* ametumia mbinu za taashira, istiari na tashbiha katika mashairi yake mengi.

ii. Msanii ametumia tamathali za taashira, istiari na tashbiha kwa mwelekeo mwema na kwa kufana, ili kuwasilisha dhamira yake.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Ni machache yamezingatiwa kuhusu dhana hizi istiari, taashira na tashbiha kwa kina katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Pili, dhana hizi zitaleta uelewa zaidi wa mashairi katika *Sauti ya Dhiki*. Jambo lingine ni kuwa diwani hii ya mashairi imeandikwa katika mazingira ya jamii ya Kenya, hivyo kuna haja ya kujua dhana hizi katika mazingira ya mshairi. Hili lafafanua jinsi tamathali hizi zinavyotumika katika jamii kimaana. Kutakuwa na uelewa wa kwa nini azitumie. Pia kutoa majukumu ya baadhi ya mbinu za uandishi katika diwani *Sauti ya Dhiki*, pamoja na kuwapa wengine shauku za kuchunguza mbinu zingine za tamathali alizotumia mshairi.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Mshairi ametumia mbinu nyingi za lugha au tamathali za semi ili kuboresha, kufafanua na kufanya imara kinachorejelewa, na pia kupitisha ujumbe wake kwa jamii. Hata hivyo tumeamua kuchanganua semi tatu pekee ambazo ni istiari, taashira na tashbiha. Tumeshughulikia dhana hizi tatu katika mashairi ishirini kati ya arubaini ambayo ndiyo tumechagua kwa kuwa yana tamathali hizi za semi.Mashairi haya ni ‘N’shishiyelo ni Lilo’, ‘Jipu’, ‘Siwati’, ‘Mamba’, ‘Ukamilifu wa Mja’, ‘Mnazi:Vuta N’kuvute’, ‘Telezi’, ‘Semani Wenye Kusema’, ‘Muwerevu Hajinyowi’, ‘Ah:Mwenzangu’, ‘Mamaetu Afrika’, ‘Jana na Leo na Kesho’, ‘Usiniuwe’, ‘Mambo Yana Mambo Yake’, ‘Watiliye Pamba’, ‘Wasafiri Tuamkeni’, ‘La Mjini na La Shamba’, ‘Ndiya Panda’, ‘Kichu Hakiwi ni Uchu’ na ‘Zindukani’.

### 1.6.0 Msingi wa Nadharia

Nadharia tuliyoitumia ni ya uhakiki wa mtindo. Kwa mujibu wa Mbatia (2001), nadharia ni mfumo wa kimawazo wenye kanuni mahususi. Nadharia inatoa mwongozo wa jinsi ya

kushughulikia na kuhakiki fasihi. Mwongozo huu wa nadharia unajumlisha vigezo, taratibu na mikakati ya kuainisha, kufafanulia na kuchambulia tungo za kifasihi. Msingi wa nadharia uliwekwa na wanafasihi wa kipindi cha urasmi. Nadharia tuliyoitumia kufanya hayo ni ya zamani sana nayo ni ya uhakiki wa mtindo. Kulingana na Barry (2002:205), nadharia hii iliibuka kutoka nadharia ya balagha ya zamani za akina Aristotle na Cicero katika nyakati za Uyunani na Urumi. Hawa walithamini jinsi ya kuzungumza, kupanga mjadala, kutoa na kuwasilisha hotuba. Naye Wamitila (2008) asema nadharia ya balagha katika jadi zizi hizi za Kiyunani na Kirumi ilithamini jinsi ya kuzungumza au kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi. Wamitila aendelea kusema kuwa nadharia hii ina makundi matatu makuu ambayo ni balagha ya kisheria / lengo, balagha ya kiutetezi /kihukumu na balagha ya kiushawishi au kisifa. Wamitila asema iliishia kukua na kuingia uwanja wa kitaalam.

Wananadharia Aristotle na Cicero walijihusisha na ufafanuzi wa matumizi ya lugha katika masimulizi, uteuzi wa maneno, mpangilio wake na namna ya kuunda ruwaza. Pia walieleza matumizi ya tamathali za usemi na mbinu nyingine za kilugha ili kuleta athari kubwa. Waliochangia mwelekeo huu wa kihakiki wa mitindo ni wana urasimi wa Kirusi na wana umuundo. Wana urasimi wa Kirusi na wana umuundo kwa mujibu wa Wamitila (2002) hushikilia kuwa lugha anayoipata mtu huwa matokeo ya maingiliano ya kijamii ambayo kwa vyovyote vile huwahusisha wazungumzaji binafsi. Wamitila anaieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii. Yaani ishara huwa na athari kubwa juu ya maudhui. Kiashiria hakiwezi kuwa funge. Mawazo haya yalitokea baada ya upanuzi wa mwelekeo wa kihakiki wa mitindo na kuchangiwa na dhana ya uchimuzi na ile ya lugha ya kishairi. Mwelekeo huu wa uhakiki wa mtindo kama asemavyo Wales (2001:437)

ulianza kuenea Uropa baada ya kuchapishwa kwa kitabu cha Bally (1909) *Stylislique* na cha Pitzer (1948) *Linguistic And Literary History.* Ulienezwa hadi Uingereza na Marekani na watu kama Halliday na kupanuka kutoka ufinyu wake wa kutumia vipengele vya kisarufi ambavyo ni vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia na ulianza kutumiwa katika aina nyingine za kifasihi kama riwaya na tamthilia.

Baada ya mpanuko huu wa miaka ya 1980 waandishi kama Leech na Short (1981), Barry (2002) na Simpson (2004) waeleza kuwa matokeo yake yalikuwa umitindo mpya. Huu mwelekeo mpya wa uhakiki wa mtindo unazingatia mengi. Hivyo ni vigumu mwanafasihi kujua njia moja ya kueleza dhana hii au kufanyia uchunguzi wake. Simpson (2004) ameorodhesha na kufafanua mambo ya kimsingi ambayo hushughulikiwa na kuchunguzwa katika kazi zozote za kifasihi panapotumika mwelekeo huu wa uhakiki wa kimtindo. Wamitila (2008) aliyaeleza zaidi mambo haya. Mambo haya ni: lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo, muwala, mshikamano na mtindo na mazungumzo na mbinu za uwasilishaji, usemi na mawazo.

### 1.6.1 Lugha ya Kitamathali na Mtindo

Lugha ya tamathali na mtindo imeshughulikiwa na wahakiki wakiwemo Kuhenga (1977) na Wamitila (2008) kati ya wengine. Kuhenga (k.h.j) katika uainishaji wake wa tamathali za semi aliibuka na vigezo vya mlinganisho wa hulka, semi za kilinge, za milinganisho wa mwigo na za vitumbuizo vya maneno.

Naye Wamitila (2003) asema ya kwamba katika ushairi aghalabu maana huwa inawasilishwa na mitindo ya kitamathali bali sio ule wa moja kwa moja. Hivyo, katika kitabu chake (2008) anaeleza haja ya kujumlisha tamathali au rasamu.Aliainisha haya katika makundi manne makuu ambayo ni tamathali au rasamu za kisentensi, tamathali/rasamu za tafkira, tamathali za kimaeneo na tamathali/au rasamu ya sauti. Wamitila amejumlisha mambo haya ili kuleta mtindo wa uandishi wa mwandishi mbali na kuiremba lugha. Pia ni kwa kuwa tamathali hizi hutumika katika mazungumzo ya kila siku. Hivyo ni ukawaida lugha kwa kiwango kingine. Vilevile hutumika kuleta maana mbalimbali hasa katika ushairi.

Ili kuwa na mtindo usio wa moja kwa moja kueleza maana, mwandishi anatumia tamathali chungu nzima kama tashbiha, istiari, taashira, ritifaa, tanakali za sauti na kadhalika. Hata hivyo, wanamitindo wamezingatia na kutoa nafasi kubwa kwa istiari na taashira kwani zinakuwa na ubunifu mkuu katika jamii wa kulinganisha vitu vyenye sifa wanazoelewa. Kwa mfano, simba na mtu mkali. Vivyo hivyo mazungumzo ya kila siku yamejaa tamathali, hivyo kuna uhakika kuwa baadhi ya maana katika lugha nyingi kuwa na asili yake kutoka tamathali za usemi.

### 1.6.2 Uteuzi na Mtindo.

Kila mwandishi huwa na uhuru wa kuchagua msamiati ambao angetaka kuutumia katika kazi yake. Huu unakuwa ndio mtindo wake ambao wanamitindo hawana budi ila kuzingatia kwa makini. Mwandishi anaweza kuamua kutumia maneno mafu, ya kale, lahaja au sajili fulani, au anaweza pia kutumia lafudhi. Uteuzi wa mwandishi huongozwa na kaida fulani za kiutanzu au mtindo wa kibinafsi wa mwandishi. Jambo lingine linaloweza kuchangia uteuzi wa msamiati ni

mandhari, mbinu za fasihi simulizi, mada na walengwa. Mambo haya yanachangia uteuzi wa msamiati na vile vile yanakuwa ni vipengele vingine vya kimtindo.

Ingawa vipengele vilivyotajwa hapo juu huchangia mtindo, huenda mwandishi asitumie vyote kwani kama asemavyo Simpson (2004) kila mtunzi huwa na malighafi ya lugha kadhaa lakini huteua kutumia mojawapo badala ya mengine katika muktadha mahususi. Kwa kufanya hili, mwandishi huwa na lengo la kuleta athari kwa msomaji ili apate ujumbe aliyodhamiria mwandishi. Hili wanamtindo hulihakiki na kuliweka wazi.

### 1.6.3 Sarufi na Mtindo.

Suala la sarufi na mtindo linajikita katika miundo ya kimofolojia na kisintaksia. Mtunzi anashughulikia suala la sarufi kwa mujibu wa utanzu kwa mfano, katika shairi mshairi hutumia mbinu za kimofolojia kama zile za inkisari, mazda na tabdila. Pia hupendelea lugha katika viwango vya virai na vishazi ambavyo hupangwa kinyume na kaida za sarufi kuvunjwa vunjwa. Haja ya kukiuka sheria za kimofolojia ni kupata urari wa vina katika ushairi na pia kupata utoshelezaji wa mizani katika mishororo. Kutokana na hayo yote ni vizuri mhakiki wa kimtindo ashughulikie mambo haya yote ili aonyeshe athari yake kwa muundo na maana ya kazi ya fasihi au matini yenyewe.

### 1.6.4 Usimulizi na Mtindo

Suala lingine la uhakiki wa kimtindo kama asemavyo Simpson (2004) ni kutathmini muundo wa kisimulizi katika matini husika. Hili huhusika na masuala ya ploti na msuko. Suala la usimulizi

linahusu mpangilio wa matukio katika hadithi na jinsi yanavyoendelezwa. Usimulizi wa hadithi hupitia sehemu tatu  mwanzo, mwili na mwisho ambao ni utatuzi.

Mtindo uu huu hufuatwa katika mashairi mengi hasa ya kale kama  Utenzi wa Tambuka ambapo wana mwanzo wa kushukuru Mungu, kiini cha kueleza yaliyomo na mwisho ambao huwa na utatuzi. Abdilatif katika diwani yake ana mtindo huu ambao wanamitindo katika uhakiki wao hawawezi kupuuza.

### 1.6.5 Uchimuzi na Mtindo

Uchimuzi ni matumizi ya lugha kwa namna inayofanya kitu kinachozungumziwa kutokea kwa uwazi zaidi. Uchimuzi unaweza kujitokeza katika kiwango cha kinstaksia au kisemantiki, maneno fulani hupewa maana tofauti au kutumiwa kwa njia ambayo ni tofauti na ile ya kawaida au maana tofauti na ile imezoeleka.

### 1.6.6 Mtazamo, Itikadi na Mtindo.

Dhana za itikadi na mtazamo hukaribiana sana maana itikadi hutokana na mtazamo na hata mtazamo huleta itikadi ya mwadishi.Itikadi ina asili yake kwenye nadharia ya Umaksi na hurejelea imani, msimamo wa mwandishi unaojitokeza katika kazi fulani. Mtazamo nao hutumiwa kurejelea mkabala wa mwandishi anaousema. Mkabala wa mwandishi huchochewa na itikadi na msimamo wake kuhusu jambo fulani, mtu au hali. Simpson (2004) asema njia bora ya kutathmini itikadi na mtazamo katika kazi ya fasihi ni kuchukulia kana kwamba unataka kupiga picha fulani. Kisha mwandishi anaangazia kazi yake katika sehemu au vipengele mbalimbali vinavyoelekeza mtazamo na itikadi.

Mambo hayo mawili hudhihirika kutokana na uteuzi wa wahusika, mandhari, maudhui na vilevile kwa njia kuu matumizi ya lugha. Ili mhakiki wa kimtindo aweze kuchanganua kazi ya fasihi lazima aiangalie kwa makini kupitia vipengele vilivyotajwa ambavyo huvidhihirisha.

### 1.6.7 Mazungumzo na Mbinu za Uwasilishaji wa Mawazo

Hapo mhakiki hutumia mazungumzo ya wahusika na mawazo yao ambayo yamewasilishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali. Uwasilishaji huu huenda ukawa katika semi halisi au taarifa yaani katika nafsi ya kwanza au ya tatu maana kama asemavyo Wamitila (2008) ni nadra kupata nafsi ya pili ikitumika. Huenda ikawa na semi halisi huru ambapo alama za mtajo hazitumiki. Pia kuna usemi wa taarifa huru ambao unajitokeza kwa kuondoa maneno yanayoonyesha kuwa huo ni usemi wa taarifa. Mshairi huteua mambo haya na kuyatumia pamoja ili kufikia lengo lake.

### 1.6.8 Muwala na Mshikamano

Ni mbinu mbalimbali za kiisimu ambazo huwezesha maneno ya aya na sentensi, virai na vishazi kuhusiana na kuleta maana na mantiki iliyonuiwa. Huleta umoja na uthabiti.

Kutokana na yote yaliyo hapo juu tunaungana na Wamitila (2008) kusema kuwa, ili mhakiki aishughulikie kazi fulani ya kifasihi vyema, ni sharti achague baadhi ya vipengele vya matumizi lugha avichunguze kwani hawezi kuvimudu vyote. Hivyo tukaamua kushughulikia vipengele vya tamathali za usemi ambapo tumechukua vitatu. Hivi ni taashira, istiari na tashbiha ambazo huwa na nafasi kubwa katika nadharia ya uhakiki wa kimtindo.

Katika kazi yetu tumezingatia, lugha ya tamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, uchimuzi na mtindo na mazungumzo na mbinu za uwasilishaji wa mawazo katika kuchunguza vipengele vya tamathali za semi ambavyo ni istiari, tashbiha na taashira katika *Sauti ya Dhiki.* Ili kuvihakiki kwa kutumia uhakiki wa kimtindo kubainisha athari inayotarajiwa kuchunguzwa katika matini husika kisha kuangalia vipengele vinavyotumiwa kuafikia athari hiyo. Kwa mfano ikiwa mhakiki ameamua kuchunguza maudhui fulani kama uovu wa jamii haya ndio yatakuwa athari inayochunguzwa. Hivyo mhakiki atasoma kazi husika na kubainisha vipengele vya kimtindo vinavyochangia haya.Taratibu tuliyoifuata ni kubainisha vipengele vitatu vya tamathali za semi ambavyo ni istiari, taashira na tashbiha katika *Sauti ya Dhiki* na kuainisha athari mbalimbali za vipengele hivi na kuzingatia mchango wake katika diwani ya *Sauti ya Dhiki.*

## 1.7 Yalioandikwa kuhusu somo kwa jumla

### 1.7.1 Istiari, Tashbiha na Taashira kwa jumla

#### 1.7.1.1 Istiari

Kama asemavyo Kuhenga (1977) istiari ni tamathali ya semi ambayo ni kitu, matendo ya kitu au vitu vyenye hulka mbalimabali hulinganishwa na hali sawasawa ya kufichuliwa kwa hisia tu. Kuhenga (k.h.j) aendelea kusema neno istiari lilizaliwa kutoka neno sitiri lenye maana ya ficha au funika. Hivyo istiari ina maana ya namna ya kifuniko au kitu chenye kuficha, kwa mfano katika sentensi hii:

Starehe kamili duniani ni paka mweusi katika giza la usiku.

Katika sentensi hii paka mweusi amelinganishwa na starehe kamili duniani. Mambo haya ya starehe duniani ni ya nadra sana kama ilivyo vigumu kumwona paka mweusi gizani. Ni shida kumwona paka wa rangi hii gizani ambalo lenyewe ni leusi.

Kineene wa Mutiso (2005) asema istiari ni mbinu ambayo kwayo kitu, matendo ya kitu au vitu vyenye tabia inayofanana hulinganishwa. Asema mtunzi hulinganisha kitu kimoja na kingine bila kutumia vilinganishi kama vile, ja, kama, kama vile n.k. Kineene aendelea kusema istiari ni mbinu ambayo mtunzi hulinganisha vitu kwa kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia. Asema istiari hujenga taswira au picha fulani.

Naye Msokile (1993) asema istiari hutumika katika hadithi kwa njia iliyopanuka zaidi. Asema maana ya masimulizi hujitokeza katika masimulizi mengine. Ametoa mfano wa hekaya na hurafa ambayo asema huwa katika kiwango cha chini cha istiari. Hata hivyo, akiri hizi hadithi ni istiari kwani hutoa masimulizi kwa kutumia wanyama kama wahusika na kila mnyama humwakilisha binadamu. Pia matendo ya wanyama wahusika husimamia matendo ya binadamu. Hivyo masimulizi yote ni istiari.

### 1.7.1.2 Tashbiha

Tashbiha kama asemavyo Msokile (1993) ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha vitu vitatu ambavyo ni kizungumziwa, kifananishi na kiungo. Kwa mfano katika mshororo huu:

> "Ua lichanue kwangu, kama koja lichanue."

Hapa kizungumziwa ni ua, kifananishi ni koja na kiungo ni kitendo cha kuchanua.

Naye wamitila (2004) asema tashbiha ni misemo ya kilinganishi ambayo hukieleza kitu au sifa zake kwa kulinganisha na kingine ili kuikuza sifa yake. Aendelea kusema kimsingi, ufaafu wa tashbiha hutegemea msingi wa picha au taswira na istiari inayofumbatwa na msemaji mwenyewe. Atoa mfano “Farida ni mrembo kama tausi” na kusema kuwa tunapomchukua ndege aitwaye tausi: mvuto wake wa sura, rangi zake na mwendo wake, na kuzifananisha na urembo aliyo nao Farida, kwa kiwango kingine tunamwangalia anayezungumziwa kama tausi. Wamitila (k.h.j) asema huu ndio msingi wa tashbiha. Aendelea kusema kwamba tunaweza kuangalia tashbiha kitaalamu kwa njia mbili kuu. Kwanza, usemi wa kilinganishi ambapo vitu viwili hulinganishwa.Pili, usemi wa kilinganishi ambao unafumbata maana fulani yaani dhima yake haiishi kwenye kilinganishi tu. Njia hii ya pili ndiyo msingi wa kueleza tashbiha kama mojawapo ya tamathali za semi. Hii ndio sababu ya kuangalia sifa za tausi ili kuweza kuelewa hasa msemaji anaposema: Farida ni kama tausi alikuwa anamaanisha ni mrembo au ana mwendo wa maringo. Dhima ya tausi kufananishwa na Farida ni mojawapo ya hizi. Mzungumzaji ndiye ajua.

Naye Kuhenga (1977) asema tashbihi ni mtindo wa kiuneni wa kifani ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au hufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti. Huwa na mfanano wa hali ya utendaji au maumbile mathalani sura, rangi na jinsi ya kujimudu. Kuhenga (k.h.j) aendelea kusema tashbiha ni neno ambalo limezaliwa kutoka kwenye neno shabihi. Maana ya neno kushabihi ni kufanana au kulingana na, kuwa sawasawa na kulanda. Mifano ya ulinganisho kama huu ni:

(a) Afya mwilini ni kama mafuta katika utambi wa taa.

(b) Watoto walimfuata mama yao nyuma kama vifaranga wa kuku wanavyomfuata mama yao.

Mfano wa kwanza unafananisha afya ambayo humsaidia binadamu kuweza kufanya mambo au kazi bila matatizo yoyote hivyo hujipa riziki au nuru maishani na mafuta ambayo husaidia utambi kuendelea kuwaka na kutoa nuru. Mfano wa pili unafananisha kule kufuatwa kwa mama na watoto wake kwa kila kitu, pengine katika tabia matendo na vile vifaranga wanavyo mfuata mama yao aendapo kukwangura mchanga wapate chakula.

Mwandishi mwingine ambaye ameieleza tashbiha ni Leech (1969) asema tashbiha huwa na maana ya juu juu ikilinganishwa na jazanda ambayo huwa na maana ya ndani . Hata hivyo Leech (k.h.j) asema tashbiha inaweza kudondoshwa kutoka kwa jazanda. Ametoa mfano wa jazanda "The ship ploughs the waves (meli huchimba mawimbi) na kutoka kwake akaunda tashbiha "The ship goes through the waves like a plough ploughing the land "(meli huchimba mawimbi kama vile plau huchimba shamba). Hata hivyo asema tashbihi huwa wazi kuliko jazanda kwa kuwa ina umahususi katika kulinganisha kwake ilhali jazanda imejaa utata.

#### 1.7.1.3 Taashira

Kuhenga (1977) asema neno taashira limetokana na neno la Kiswahili ishara. Asema maana ya taashira ni yenye kutoa ishara, alama, kidokezo au kufidishwa kitu au chombo cha utendaji huwakilisha mtendaji. Nne, mahali kitu kilipotengenezwa huwakilisha tendo. Kuhenga (k.h.j ) ametoa mifano hii ya taashira katika kifungu hiki:

> Baada ya mwito wa kuanzisha kijiji cha ujamaa huko Msata, kulitokea mkikimkiki mkubwa. Kukawa huku shoka lakata miti, jembe lang'oa magugu, mitungi na maji na mwiko na kuta za nyumba. Si muda mwingi kijiji kikajengeka. Mawingu ya mvua yalipotuna, watu wakawa mashambani wakishika jembe, kila siku hadi jua linapomezwa na mawingu. Wakati wa msimu ulipofika watu wakaandamana sokoni na magunia ya nafaka. Baada ya kukunja noti, Wananchi wakakimbilia madukani kujinunulia mashuka ya Merikani, kanzu za China na kofia chapa Japani. Wapenda mambo ya starehe wakanunua radio, asubuhi wakifurahia nyimbo wafunguliapo akina Salum Abdalla au akina Mbaraka Mwinshehe ili mradi kila nyumba ikawa na furaha.

Katika kifungu kilichoko hapo juu mwandishi ametumia taashira kadhaa zikiwa na maana tofauti kwa mfano, shoka la kukata miti liliwakilisha watu wenye kukata miti, jembe la kung'oa magugu linawakilisha watu wanaong'oa magugu. Mitungi, mwiko na kuta za nyumba ni wachota maji na waashi wa kujenga nyumba mtawalia. Hizi ni baadhi ya taashira ambapo vitu fulani vinasimamia watu wanaofanya kazi tofauti tofutti. Vitu hivi ndivyo ishara.

Ishara kama asemavyo William H. (2003) ni kitu chenye maana nyingi. Aendelea kusema kwamba ishara ina maana isiyokomea ile moja tu ambayo imepewa kitu kimoja mahususi. Ishara hizi mara huleta maana katika kazi kimuktadha ambazo hazina maana ya asili au ile inayojulikana katika hali ya kawaida. William (k.h.j) aliibuka na aina mbili za ishara ambazo ni

zile zinajulikana ulimwenguni mzima kama vile nuru kumaanisha ujuzi au fuvu kumaanisha kifo. Pili kuna ishara zinazoundwa na kupewa maana kulingana na jinsi mwandishi amezitumia.

Naye Northrop Fyre na wengine (1985) wameweka ishara katika makundi matatu ambayo ni ishara za kiasili ambazo husimama kama vibadala vya mawazo ambayo kawaida watu huhusisha navyo kama vile nyota kuonyesha tumaini. Aina ya pili ni ile ya kawaida ambayo huwakilisha maana ya vitu fulani katika jamii fulani mahususi. Aina ya tatu ni ishara za kazi ya fasihi au uandishi. Hizi huundwa kutoka zile za kiasili na kawaida ambazo huongezwa maana au maana hupanuliwa katika kazi za kimsingi. Huu ndio msingi wetu katika kuhakiki taashira katika diwani ya S*auti ya Dhiki*.

Leech (1969) asema taashira ni ile maana ya kibunifu ambayo inahamishwa kwa kitu kutoka ile ya kawaida. Ametoa mfano wa taa kumaanisha ujuzi, nyota kumaanisha iliyothabiti au imara, ndimi za moto kumaanisha hisia kali. Anasema baadhi ya taashira huwa ni jambo la kweli na katika ukawaida wake. Ametoa mfano kuwa jiwe liviringikalo mlimani halipati kuvumwani kumaanisha mtu ambaye hatulii katika kushughulikia jambo fulani huwa jambo hilo halifaulu. Pia chombo kilicho kitupu huwa na kelele nyingi. Leech (k.h.j) amesema ingawa jambo hili ni la kawaida litachukuliwa kuwa ni taashira maana hakuna sababu ya kiisimu inayoeleza maana ya mwelekeo wa maisha au kwa nini neno haliwezi kuchukuliwa kwa maana yake ya kawaida na kuwa taashira. Pia akiri ni vigumu kusema vipi na lini neno lichukuliwe na maana ya ukawaida wake au maana ya kiubunifu. Hata hivyo asema kuna ulinganisho wa kiasili na wa kimuktadha ambao huzua maana ya taashira. Aendelea kusema wakati mwingine

waandishi huunda taashira zao badala ya kutumia zile za kawaida au zile zimekuwa zikitumika kwa muda mrefu.

Naye Day-Lewis (1947) alisema kuwa taashira katika ushairi ni sehemu ya ukuaji ulio hai. Kile mshairi wa kisasa anachotafuta katika taashira ni upya, mkazo na hisia zenye nguvu za kusisimua. Baada ya haya kutokea, kunapatikana kitu ambacho hatukuwa nacho mbeleni. Day-Lewis (k.h.j) atajapo mkazo anamaanisha kukipa kitu makini na maana kuu kikiwa katika hali yake ndogo. Yaani kitu kidogo chenye maana ya kawaida hupanuliwa maana na kuwa ya hali ya juu kweli. Maana hupatikana kutokana na kukaribiana na kuwa na uhusiano wa ishara na kirejelewa. Msisimko ni nguvu za ishara katika shairi ambazo huibuka kutoka kwa binadamu akihusishwa na hisia za shairi lenyewe. Hili jambo hupimika tu kibinafsi kwani kila binadamu hupata hisia fulani na za kiwango fulani kutokana na ishara na hisia zinazoletwa na shairi.

Day-Lewis aendelea kusema ishara katika ushairi si lazima iwe taashira kabisa kwa kuwa zinadhihirika na hisia zinazoibuka kutoka muktadha wao hivi kwamba kila msomaji huathirika kutokana na tajriba zake hivyo huzipa maana tofauti na mwingine. Ameutoa mfano wa ishara ya neno '-eupe' ambalo huwa ni ishara ya amani huenda likapata maana nyingine nyingi kulingana na maana aliyokusudia mtunzi.

### 1.7.2 Yaliyosemwa kuhusu somo katika kazi mbalimbali

Ingawa mengi kuhusu mbinu hizi tatu hayajasemwa katika *Sauti ya Dhiki*, mengi yamesemwa kwingine kuhusu dhana hizi tatu. Kuna waandishi wameandika mengi kuhusu mashairi mbalimbali. Mbinu hizi zimetumika sana hasa katika mashairi ya Kiswahili na Waafrika

wakirejelea tajriba zao ili ujumbe wao ueleweke na walengwa wao. Kwa mfano Abdulaziz (1979) ameonyesha kuwa, Muyaka ametumia istiari ambapo dunia imefananishwa na mti ambao umekauka na kuoza. Asema:

"Dunia mti mkavu ,kuimbe usiuleme"

Mtiwe 'ni mtakavu'

hivi kwamba hauna nguvu tena za kusaidia binadamu. Pia dunia imefananishwa na mwendo wa ngisi.

'Dunia ni mwendo wa ngisi'

Yaani dunia huenda mbele na kurudi nyuma kama vile samaki huyu (ngisi) hufanya.

Katika ubeti wa tatu dunia imeitwa kitu dhaifu. Imelinganishwa na kitu dhaifu ambacho hakiwezi kumfaa binadamu.

Mbinu nyingine ambayo imetumiwa katika shairi lili hili ni taashira. Katika ubeti huu mshairi asema:

Dunia mti mkavu, kiumbe siulemele

Ukaufanyia nguvu, kuudhibiti, kwa ndole,

Mtiwe ni mtakavu, mara ulikwangushile

Mishororo hii mitatu yatoa ishara ya mti uliosimama lakini ni mkavu umeoza hivi kwamba yeyote ajiegemeaye kwake huanguka. Pia katika mshororo ulio hapa chini ametumia tashbiha


"kumbuka na uvundifu, ujapo ni kama ndwele"

Hapa amaanisha kuharibikiwa na dunia ni kama maradhi ambayo yaweza kudhoofisha, kuua au kufilisi (hasa wakati mtu anatafuta matibabu).

Mwingine ambaye ameshughulikia istiari, taashira na tashbiha ni Lugwiri L. katika tasnifu yake ya uzamili (2011) akitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Amezishughulikia hizi katika utenzi wa Tambuka. Ameangazia dhana hizi tatu kwa kuonyesha aina zake na jinsi zimechangia kueleza dhamira na kufikisha lengo la mshairi kwa lengwa wake. Kuna zile mbinu ambazo zilitumia wanyama katika ulinganishi kwa mfano simba kurejelea nguvu zake yaani mtu analinganishwa na mnyama huyu katika tashbiha, pia nyoka, paa, chui, mbuzi, nyati na kadhalika. Hawa ni wanyama ambao wamo katika mazingira ya Waafrika. Waliwaelewa tabia zao na hivyo walitumika kuunda tamathali mbalimbali za semi. Mbuzi alilinganishwa moja kwa moja na wasio na mwelekeo; chui akiwa na maana ya maisha ya siri na mbio na vilevile kutokata tamaa. Hili limetusaidia katika uelewa wa zile zilizotumika katika *Sauti Ya Dhiki,* hata hivyo mielekeo yake kimaana huenda ikawa tofauti na mengine kufanana kwa mfano ndovu kutajwa kumaanisha nguvu katika *Utenzi wa Tambuka.* Ndovu ametumiwa kwa maana iyo hiyo katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* katika shairi 'Kichu Hakiwi ni Uchu'. Pia wanyama wametumika kuunda istiari mfano simba, chui, mbwa na kadhalika. Vile vile sifa zao ndizo anarejelea zaidi. Pia amerejelea istiari za kimaumbile ya kiasilia. Mfano jangwa, milima na mabonde, giza na baridi. Hizi ni istiari za usuli. Milima imetumika kuashiria jeshi la Waislamu. Kwingineko mlima ukiwekwa pamoja na vilima kumaanisha ugumu au shida. Giza hurejelea uoga au kushindwa. Nayo baridi hurejelea upweke kutokana na sifa ya watu kujikunyata wakati wa baridi. Pia mshairi ametumia kesho kuashiria maisha baada ya hapa ulimwenguni.

Mwandishi mwingine ambaye ameshughulikia mbinu hizi ni Coward D. (2002) ambaye ameshughulikia taashira na kusema kuwa, katika mfumo wa mawazo wa taashira za ushairi, maneno hubadilishwa na kukoma kuwa njia ya kutoa maana tu na kuwa ukweli halisi ambao umekuwa zaidi ya irabu na konsonanti zao. Maneno haya huwa ndio kitendo na kitendwa katika ushairi. Maneno haya hupangwa na kuleta dhana na mawazo kama sigareti inavyoweza kuleta mduara wa moshi. Huu aueleza kuwa mwanzo wa mshairi kinyume na tajriba au mawazo ya awali au hisia za mtunzi. Akirejelea taashira asema wanataashira walipoanza kuitumia ilipitia mabadiliko katika jadi tatu na kuleta mtindo mpya wa ubunifu wa kiasili wa sanaa na wanasanaa. Hili lilileta ubinafsi, ubunifu wa hali ya juu na uhuru wa mtindo.

Mbinu hizi zimeshughulikiwa na Mlacha na Hurskainen (1995) ambao wanasema kuwa ishara za kiisimu/ lugha huwasilisha uhusiano kwa njia tatu katika mazingira yake: kwa mzungumzaji au mzungumzi wa ishara, kwa msikilizaji/ mpokeaji na kwa mada inayozungumziwa. Wakimnukuu Karl, Buhler via Euginio (1981:53) akiwa na mchoro huu:



Mlacha na Hurskainen (1995) wasema ishara ni kionyeshi cha uhusiano na mada; ni dalili inayowasilisha ujumbe fiche kuhusu anayetumia ujumbe huo. Hiki kionyeshi ndicho kinatokea kwa mpokeaji ili aweze kutenda kwa njia fulani. Hizi ishara zinaweza kuwa ni istiari, tashbiha au taashira. Hili limetusaidia kujua kuwa kila mada huweza kuwa na maana tofauti ikiwa ishara itapokewa na wapokeaji tofauti. Hivyo ni kusema mhakiki ana uhuru wa kuhakiki kazi binafsi.

Naye Harries (1962) aonyesha mbinu hizi tatu kama zilivyotumiwa na Mgeni bin Fiqihi katika baadhi ya beti kutoka utenzi wa  Ras il Ghuli. Kwa mfano neno mwewe katika ubeti wa arubaini limetumika kumaanisha mtu aliyetenda maovu au kunyima watu haki kama mwewe amtendavyo kuku. Ameonyesha tashbiha ya watoto kuchinjwa kama mbuzi; mbwa kurejelea kiongozi ambaye ana sifa za mbwa asiyejua mema. Hii ni taashira katika ubeti  wa saba, arubaini na mbili, sitini, sitini na sita. Vilevile ametumia  asadi (simba) kumaanisha ukali na nguvu za vijana wake.

Mwandishi wa Ras il Ghuli ametumia tashbiha chungu nzima kama alivyonukuliwa na Harries (1962)  zikitumia wanyama na vitu vingine kama jua. Katika ubeti  wa mia na saba chandarua kinametameta kama jua. Ubeti wa mia ishirini na nane sauti ya mvinyo ikiteremka kooni ilikuwa,

"kama jiwe twaani, mtama au shairi".

Tamathali hizi za semi  zimeshughulikiwa na Kineene wa Mutiso (2005). Yeye asema tashbiha ni pale kitu kimoja, vitu au hali mbili na hata zaidi hulinganishwa na kitu kimoja au vitu ama hali mbili na hata zaidi. Kwa kutumia vilinganishi kama, ja, mithili (ya), mfano (wa), kama –fanana na, na vile vile sawasawa na. Kufanana huku huwa ni kwa ushabihiano kwa hali ya utendaji au maumbile. Asili ya neno lenyewe ni shabihi yaani kufanana. Ameonyesha mifano katika utenzi

wa Hamziyyah kuwa Mtume Muhammad amelinganishwa na bahari na watu mwingine vidimbwi kuonyesha ukuu na udogo wa watu hawa mtawalia. Uso wa Muhammad umelinganishwa na mng’ao wa jua, Korani tukufu na kioo, mkono wa Muhammad na mfuriko kuonyesha wingi wa rehema. Haya yamejaa tele katika kasida ya Hamziyyah.

Istiari ni mbinu nyingine ambayo imetumika katika utenzi huu .Vilevile ameonyesha taashira ambayo Kineene (k.h.j) amesema ni kitu au tukio linaloficha maana au hisia mahususi. Ni ishara, alama, kidokezi, dalili na hata neno fulani ambalo hutumiwa kuwasilisha kitu ambacho hatungetaka kukitaja moja kwa moja. Kwa mfano katika kasida ya Hamziyyah mito na chemichemi za mafursi zilikauka; kwa mioto, kichwa cha Mtume kuelekea mbingu. Haya yote yanaonyesha upekee wa Mtume na ndiye atakayekuwa mkuu zaidi wa wote. Huenda istiari katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* zikatofautiana na za utenzi huu wa Hamziyyah kwa sababu vipindi ni tofauti na vile vile waandishi. Pia kwa sababu dhamira za kazi ni tofauti.

Pia Nabukonde (2011) katika tasnifu yake ya uzamifu ameshughulikia kwa kina dhana ya taashira katika mashairi nchini Uganda akitumia nadharia ya uhamisho. Ametumia maneno mbalimbali yakirejelea dhana mbalimbali, kama vile mti kurejelea maisha ya binadamu, damu ambayo huashiria mauaji, milima na vijilima kuashiria ardhi au nchi; jeshi na polisi ni ishara ya mauaji katika shairi “Men Love Chocolate’’. Pia katika shairi hilo hilo maneno muziki, nyimbo na ngoma yanaashiria maisha ya furaha iliyokuwa vijijini.

### 1.7.3 Yaliyosemwa kuhusu somo katika Sauti ya Dhiki

Katika kupitia kazi mbalimbali za uandishi tumepata mengi yamesemwa kuhusu *Sauti ya Dhiki* lakini si mengi yamesemwa kuhusu mbinu hizi tatu; taashira, istiari na tashbiha kama zilivyotumika katika *Sauti za Dhiki*. Yaliyosemwa kuhusu mashairi haya ni kwamba mwandishi aliyaandika akiwa kifungoni. Mengine yalisemwa kuhusu mashairi haya yamesemwa na baadhi ya watu kama Chacha (1980).

Chacha (k.h.j) ametoa historia ya kitabu chenyewe na kusema kwamba mkusanyiko wa mashairi katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* ni zao linalotokana na kufungwa kwa Abdilatif. Kifungo hiki cha miaka kilijaa dhiki nyingi. Chacha (k.h.j) asema wahakiki wajiuliza kama kitabu hiki kilifaa kuitwa *Sauti ya Dhiki*. Asema kuna hoja zinasema kuwa kwa sababu Abdilatif alikuwa kifungoni lazima angetoa kilio chake kwa sauti ya ukali huku akiendelea kuwapinga hao wenye nguvu ambao wamemgandamiza. Chacha (1992) asema anakubaliana na Bi. Matteru anaposema kuwa *Sauti ya Dhiki* ni utetezi; ni maombolezo; ni sauti ya shime; ni mjadala wa kitulizo na kuliwaza.
Kile anachofanya Abdilatif kama asemavyo Chacha (1980) ni kuelimisha umma wa ulimwengu wa tatu kuhusu jukumu na dhima yao katika harakati za kujikomboa. Anatoa mfano katika shairi "Semeni Wenye Kusema" ubeti wa kwanza.

Chacha (k.h.j) ameshughulikia baadhi ya mashairi ya *Sauti ya Dhiki* na kuonyesha maudhui mbalimbali kwa mfano maudhui ya kuzindua akili ambayo yapo katika mashairi "Telezi", "Ndiya Panda", "Mambo yana Mambo Yake" na "Mamaetu Afrika". Pia kuna maudhui ya kujigamba. Maudhui mengine ni utetezi wa wengine na ametumia shairi "Usiniuwe". Ameeleza kuwa kuna chama cha kisiasa KPU kilichoanza kisheria chini ya chama cha KANU, hiki chama

(KPU ) hakikutaka kuuwawa bali kilitaka kupewa nafasi hata kama hakingeshirikiana na KANU. Uchambuzi wa Chacha umetusaidia kuelewa kwa undani mbinu za uandishi alizotumia mshairi, kama sitiari kwa mfano mwana anayelia, pia taashira ya mtoto kutotaka kukatiziwa uhai na mama.

Chacha (1980) amegawa mashairi ya *Sauti ya Dhiki* katika makundi mbalimbali akiegemea maudhui. Ana makundi ya kisiasa, kiuchumi na maisha ya makhluki (yanayohusu itifaki za jamii na mapenzi) katika jamii, mengine yana ubinafsi wa mtunzi mwenyewe. Pia kuna yanayohusu siasa na jinsi matukio ya siasa yalivyogongana na mahusiano ya watu wote. Kwa ufupi, ameyajumlisha mashairi yote katika mafungu matatu makuu ambayo ni:

(a) Mashairi yenye msimamo wa mwandishi katika jukumu la kutetea haki na maslahi ya umma.

(b) Mashairi yenye ubinafsi na hisia zake (msanii)

(c) Mashairi yanayoonyesha migongano na mikinzano katika hisia na fikra za ndani za mtunzi.

Baadaye akayaangazia katika makundi mahususi kwa mfano mashairi aliyoyaita ya kuzindua akili kama vile “Telezi”, “Mambo Yana Mambo Yake” na “Mamaetu Afrika”. Katika mashairi haya alifafanua jazanda na mafumbo yaliopo. Katika shairi “Telezi” anaichukulia mvua kuwa vita vya ukombozi wa nchi kutoka minyororo ya ukoloni. Vita hivi vilikuwa vya muda mrefu mpaka mashujaa wakachoka. Asema vita vyaleta madhara chungu nzima kama kubomolewa kwa nyumba, kuharibiwa kwa mimea, majeruhi, hofu, umwagikaji wa damu na vifo. Ugumu wa vita unalinganishwa na ugumu wa kilimo hasa mvua inaponyesha zaidi na kufanya udongo kuwa

tope tupu. Ilibidi watu kutoroka kama vile asemavyo Chacha (k.h.j) na kama alivyoandika Abdilatif.

Kazi hii ilitusaidia kuweza kutambua tashbihi, taashira na istiari ambazo ametumia Abdulatif katika diwani ya *Sauti ya Dhiki.* Vilevile kuweza kujua kama amefikia dhamira yake ya kufahamisha walengwa wake.

Chacha (k.h.j) amehakiki shairi "Mamaetu Afrika". Amesema bara la Afrika lingali vitani kwani kuna nchi ambazo hazikuwa zimepata uhuru na zingine zilipata wa bendera tu. Nchi hizi za uhuru wa bendera zinanyanyaswa na vikaragosi na wakoloni mamboleo. Abdulatif alilia bara letu katika shairi hili. Anaonyesha maadui hawajabadilika. Ni wakoloni wakongwe wanazunguka kama mwewe azungukavyo vifaranga. Walipora mali na kutumisha waafrika kwa nguvu na kuwagawa katika makundi ya makabila. Anawashutumu vikaragosi, viongozi na wasomi teule kwa kuuacha uafrika wao na kuwa kama weupe.

Kama ilivyo katika mashairi mengine, uhakiki huu unasaidia kuelewa maudhui na dhamira ya mshairi. Pia kutambua mbinu za uandishi alizotumia mwandishi. Hivyo tuliweza kutambua pale ametumia taashira, istiari na tashbiha.

Muasya (1991) ameshughulikia maudhui kama uozo katika nyanja ya kisiasa katika mashairi 'Mamba' (uk. 10)' Mnazi' (uk. 17)'na 'Muwerevu Hajinyowi' (uk. 27). Pia maudhui ya uozo katika tabia za watu akitumia shairi 'Usiniuwe' ambapo mwana (kilinge) alia asiuliwe na mama kabla hajazaliwa. Maudhui ya kuibuka kwa jamii bora akirejelea shairi 'Jipu' na 'Mamba'.

Ingawa hatukushughulikia maudhui, haya yalitusaidia katika kuelewa zaidi matumizi ya tamathali za semi istiari, taashira na tashbiha kwani akiyafafanua anaeleza maana ya baadhi ya tamathali hizi. Kwa mfano katika shairi 'Muwerevu Hajinyowi'; maneno mbiti na mbivu ambayo yametumika kuwakilisha maudhui ya uozo katika nyanja ya kisiasa ni taashira yenye maana yasiolika au yasiyo mazuri (mbiti) na mbivu ni mambo ambayo ni kama matunda yaliyotayari kuliwa yaani ni yenye utamu. Ni mambo yaliyokubalika katika jamii.

Mwangi R. (1992) ameshughulikia suala la siasa katika *Sauti ya Dhiki*. Amehakiki mashairi "Mnazi: Vuta N'kuvute" ambalo asema ni uhusiano ulioko kati ya watawala na watawaliwa. Ni uhusiano wa mpanda ngazi na mshuka ngazi. Aseme mpanda ngazi ni kiongozi anayewakilishwa kwenye shairi hili na Badi huku mshuka ngazi ni mtawaliwa. Hawa watawala baada ya kukwea ngazi au kupanda vyeo wanawasahau wananchi na kujinufaisha peke yao. Asema mnazi ni mmoja lakini kila mtu ataka kutumia nguvu kuukwea. Kimuktadha, nafasi za uongozi ni chache lakini kila mtu ang'ang'ania ajaze.

Ameangazia mashairi mengine kama "Kenya: Twaendapi?" "Muwerevu Hajinyowi" "Semeni Wenye Kusema" na "Mamaetu Afrika". "Mamaetu Afrika" ni shairi lenye nahodha au viongozi wabinafsi wasiotosheleza mahitaji ya abiria wao. Asema kila mmoja ataka awe ndiye mshika usukani. Mashairi mengine ambayo ameangazia maudhui haya ya siasa ni "Jipu" (shairi lenye mafumbo kama asemayo Mwangi (1992); pia ameshughulikia "Mamba" na "Zindukani".

Katika maudhui ya dhiki zinazowakumba wafungwa, Mwangi (1992) ameangazia mashairi kama "N' Shishiyelo ni Lilo" na "Siwati" kueleza kwamba hatoacha imani yake na liwe liwalo.

Maudhui haya yamo katika shairi “Telezi” (uk. 24) akirejelea dhoruba zinazopatikana kifungoni. Katika maudhui ya ubepari Mwangi (k.h.j) ameangazia shairi ‘Zindukani’ (uk. 69) ambapo analaani mahusiano ya kijamii ya kukubali tabaka la wachache  na kulaza damu na kungoja majaliwa ambayo ni jasho la wengi. Pia ameangazia ‘Kichu Hakiwi Ni Uchu’ (uk 82) ambapo asema mshairi ametumia mfano wa ndovu mwenye nguvu anayeogopwa sana mwituni lakini daima atabaki mnyama na si  kwamba ni mtu ndovu kwa sababu ya nguvu zake.

Mwangi ameangazia maudhui ya mwito wa uzalendo. Amehakiki shairi “Mamaetu Afrika” na kuangazia sababu za kutosikizana kwa jamii kwani kila mtu ataka kushika usukani.  Abdilatif (1973) auliza swali la balagha katika shairi lili hili “Litawezekana lini?” Swali hili larejelea kushika usukani kwa kila mtu.Ingawa sisi hatushughulikii maudhui katika *Sauti ya Dhiki* bali tamathali za semi tatu istiari, taashira na tashbiha, maudhui haya yanasaidia kuangaza matumizi na maana za tamathali hizi kwa njia moja au nyingine kwa mfano Mwangi (1992) anapoeleza mamba kama kiongozi ametoa uhakiki wa taashira hii.

**1.8 Njia za Utafiti**

Kwa kuwa ni utafiti wa fasihi andishi, utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma mashairi mengine na vitabu vinavyoeleza na kutumia istiari, taashira na tashbiha. Hili limetusaidia kupambanukiwa na falsafa inayoongoza matumizi yake. Tumeusoma ushairi kwa jumla ili tuweze kueleza msingi wa mbinu hizi tatu. Njia ya kuchagua data yetu ilikuwa sampuli ya kusudi.Tumesoma diwani ya *Sauti ya Dhiki*  ili kupata matumizi ya lugha ya mashairi haya. Kisha tumechagua baadhi ya mashairi ambayo yametumia mbinu za istiari, taashira na tashbiha.Tumefanya hivi bila kuwa na ufahamu wa athari inayoletwa na vipengele hivi katika

kazi ya fasihi tunayoshughulikia. Baadaye tumeonyesha jinsi vipengele husika yaani istiari, tashbiha na taashira vinavyoeleza na kuendeleza athari fulani katika *Sauti ya Dhiki* kisha kuangazia jinsi mbinu; istiari, taashira na tashbiha zilivyotumika katika mashairi yote tuliyoteua kushughulikia.Tumeeleza maana ya kila moja na kuonyesha jinsi zilivyotumika ili mshairi aweze kufikia dhamira yake. Hili limetusaidia kuweka wazi  kinachozungumziwa.

**1.9 Hitimisho**

Katika sura hii tumeeleza kwa kifupi mbinu za istiari, taashira na tashbiha. Kisha tukashughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti ambayo ni mawili na nadharia tete ambazo ni mbili. Pia tulieleza sababu za kuchagua mada ambayo ni "matumizi ya istiari, tashbiha na taashira katika *Sati ya Dhiki".* Tumetaja upeo na mipaka yetu ambayo ni mashairi ishirini kutoka diwani hii ya *Sauti ya Dhiki.* Jambo lingine tuliloshughulikia ni msingi wa nadharia ya uhakiki wa mtindo ambapo kwayo tumeeleza mambo ya kimsingi ambayo huchunguzwa panapotumika nadharia hii. Baadaye tukaangazia yaliyoandikwa kuhusu somo kwa jumla kisha yaliyoandikwa katika kazi mbali mbali na katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Hatimaye tukataja njia zetu za utafiti. Katika sura ya pili tutaangazia aina mbalimbali za tamathali za istiari, taashira na tashbiha.

# SURA YA PILI

## 2.0 MSINGI WA KINADHARIA WA TAASHIRA, ISTIARI NA TASHBIHA

### 2.1 Dhana ya Taashira

Myers na Simms (1989) wasema kuwa asili ya taashira ni katika Ugiriki ikiwa na maana ya kubadili jina. Aendelea kusema taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo neno au fungu la maneno hutumika badala ya neno au fungu lingine la maneno. Neno la kinachozungumziwa husimamiwa na kitu kingine. Mbatia (2001:46) akubaliana na haya anaposema ni tamathali ya usemi ambapo kitu kiitwacho jina A kinatumiwa kutaja kitu B. Nabukonde (2011) asema taashira ni ishara. Naye William (2003) asema ishara huwa yenye maana nyingi wala sio maana moja mahususi. William aendelea kusema ishara hizi mara huleta maana katika kazi kimuktadha ambazo hazina maana ya kiasili au iliyokubalika katika jamii. Aliibuka na aina mbili za ishara ambazo ni ishara bia ambazo huwa na maana inayajulikana kilimwengu kama vile nuru kumaanisha ujuzi au fuvu kumaanisha kifo. Pia kuna ishara zinazoundwa na kupewa maana kulingana na jinsi mwandishi amezitumia.

Nao Northrop, Sheridan na Perkins (1985) wamezigawa ishara katika makundi matatu; ishara za kiasili ambazo husimama kama vibadala vya mawazo kwa mfano nyota kuonyesha matumaini. Pia kuna mfano katika utenzi wa Rasi 'IGhuli kutoka ubeti wa 3773-3784 ambapo Arege (2012) aeleza tukio la taashira. Hapa punda ni kibadala cha wasio wa dini ya kiisilamu, kuwinda punda ni kuwasaka, kuwachinja ni kuwakomesha kabisa na kula nyama pamoja kunaashiria umoja. Ishara ya pili ni ya kijamii na ya tatu ya uandishi (hii huundwa kutokana na ishara za kawaida na za kijamii). Hata hivyo neno linalosimama badala ya lingine au kinachosimama badala ya

kingine sharti kiwe na uhusiano fulani wa kimaumbile, kisifa, kisemantiki au wowote ule. Kwa mfano katika sentensi hii, “Chui amemshambulia mumewe huku wanawe wakimtazama kwa mshangao; kwa kweli Asha ameharibika.” Asha aitwa chui kwa sababu ana sifa sawa na mnyama huyu kitajriba. Ana mazoea ya kuwa mkali hivyo huenda jamii ikampa lakabu hii badala ya jina lake mwishowe.

**2.1.0 Aina maalum za taashira**

**2.1.1 Sinekidoki**

Hii ni aina ya taashira  ambayo hutumia sehemu ya kitu kusimamia kitu chenyewe. Hali hii hutokea katika methali, nahau na semi. Kwa mfano katika methali ‘mkono utoao ndio upatao’;.mkono umetumiwa kama sinekidoki ya mtu. Methali hii inamaana kuwa mtu anayesaidia wengine ndiye hupata baraka kwa mengi.

Thrall na Hibbard (1960:48) wanasema sinekidoki nzuri inafaa kujengwa kwenye sehemu muhinu au kuu ya kitu kizima. Haya maneno yamekubaliana na methali iliyoko hapo juu.Vilevile ina maana  kuwa lazima kinachotumiwa kiwe na uhusiano mkubwa na mada husika. Kwa mfano Lugwiri  (2011) atoa mifano ya kuonyesha kauli hii ambayo ni:

(i) Tunahitaji mikono zaidi kazini.

(ii) Tunahitaji tumbo zaidi kazini.

Tunakubaliana naye anaposema kuwa sentensi ya kwanza ina kuwa wazi na kubalifu kuliko ile ya pili kwani kazini ni mahali pa kufanya kazi na panahitaji watu zaidi (mikono) bali si tumbo (walaji).

Abraham (1941) anasema ingawa kwa nadra sana, kitu kizima kinaweza kusimamia sehemu ya kitu hicho. ‘Serikali imefika’ (askari wamefika ) serikali ni kitu kizima ambacho kinasimamia sehemu ambayo ni askari.

### 2.1.2 Taniaba

Hapa mtu au kitu hurejelewa kwa kutaja tabia, sifa au hali ya mtu au kitu kingine. Sifa hizi na tabia na jina linalotumiwa lazima liwe linajulikana na hadhira lengwa.Kwa mfano neno

“baba” likirejelea kiongozi katika ulingo wa siasa nchini Kenya.

‘Mwokozi atatupigania. ’Neno mwokozi linarejelea Yesu au nabii Issa,

‘Hitler’ nalo hurejelea viongozi wa kidikteta.

### 2.1.3 Lakabu

Ni neno la asili ya Kiarabu lenye maana ya sifa anayopewa mtu kwa sababu ya sifa maalum au ya upekee fulani. Mtu au kitu hupewa jina lingine tofauti na jina halisi. Jina hili husheheni sifa za kirejeleo na hutukuza athari fulani. Majina ya aina hii hutumika katika tenzi za Kiswahili kurejelea majina ya Mungu na mitume wake kwa mfano neno nuru katika utenzi wa Rasi’l Ghuli kurejelea Mtume Mohammad.


## 2.2 Mbinu ya Istiari

Myers na Simms (1989:178) wanasema kuwa dhana ya istiari ina asili yake katika lugha ya Kigiriki na ina maana ya kuhamisha au kuvusha hadi upande mwingine. Kutokana na maelezo haya istiari ina maana ya kuhamisha maana ya kimsingi au sifa za kitu kimoja hadi kingine. Kwa kulinganisha vitu au watu hawa wawili. Maana ya kimsingi hukiukwa na inayorejelewa huwa ni

ya kipragmatiki kwa mfano, maisha yamekuwa jabali. Maisha yamekuwa jabali kwa msingi wa sifa za uzito na ugumu ambao si rahisi kuondoa.

Istiari imekuwa ikitumika kwa muda mrefu tangu jadi za Urumi na Uyunani. Nyakati hizo ni tabaka fulani tu lililokubaliwa kutumia istiari. Hili lathibitishwa na Fiumara (1995:2) anaposema kuwa, katika jadi ya Urumi na Uyunani, lugha ya kiistiari ilitengewa watawala, matajiri na waajiri. Watumwa hawakuruhusiwa kuzungumza kwa lugha ya kiistiari kwani ingekuwa sawa na kupigana au kushindana na mabwana wao.

Muundo wa istiari unakuwa na sehemu tatu ambazo ni kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi. Lugwiri (2011) ameonyesha kwa mchoro ufuatao uhusiano wa mambo haya matatu. Kwa kutimia mfano wa istiari hii “Kamau ni ng’ombe” tumeonyesha maana nyingi ambavyo zinatokea kutoka kwake; hivyo maana lengwa hutegemea muktadha. Haya ni kama yalivyo katika jedwali hili:




### 2.2.0 Aina ya istiari

#### 2.2.1 Istiari Chakavu

Abrahams (1957: 64) aieleza istiari chakavu kama istiari ambayo imetumiwa sana katika lugha hivi kwamba haionekani kama istiari tena. Hii ni kwa sababu huwa zimefungamana sana na matumizi ya kawaida hivyo kupoteza ubinafsi wake. Istiari hii ikitumiwa huwa imepoteza athari za kisanii kwa hadhira. Nyingi za istiari hizi huwa katika misemo na nahau kwa mfano, meno ya msumeno, jicho la sindano, mkono wa birika mdomo wa chupa na kadhalika.Wamitila (2008) pia aita istiari hii sitiari fifi na kuieleza kuwa ni ile ambayo hutokea pale ambapo taswira ambayo zamani ilieleweka kama istiari haichukuliwi hivyo tena labda kutokana na mpito wa wakati.Istiari hii imepoteza mshitukizo ambao ni muhimu katika istiari. Mifano ya istiari hii ni uti wa mgongo,mtoto wa meza na agizia risasi.

### 2.2.2 Istiari kuu

Istiari hii ni ile ambayo hutawala kazi ya kifasihi kutoka mwanzo hadi mwisho. Dhima yake kuu ni kuwasilisha dhamira na maudhui katika kazi ya fasihi mfano katika diwani ya *Bara Jingine* ya Kithaka wa Mberia (2001) katika shairi *Mruko wa Nyuki* , mruko wa nyuki ni istiari inayorejelea waafrika ambao hata baada ya kazi ngumu ya kujikomboa kwa pamoja katika pingu za utawala wa mkoloni bado hawajapata uhuru. Wanatengana na kuzuia maendeleo barani Afrika. Mruko wa nyuki unadhihirika katika muundo wa shairi ambao umeanza kwa maneno yakiwa yamekaribiana baadaye yanatengana kiasi cha kila herufi kuwa peke yake. Hivi ndivyo waafrika walianza kwa umoja lakini baadaye wakatengana kabisa na kupoteza umoja wao.

### 2.2.3 Istiari ya kikaida

Istiari ya aina hii ni ile ambayo hufungamana na utamaduni wa jamii iliyozaa kazi ya kifasihi inayohusika. Kuna jamii ya kiafrika inayotumia usemi,'watu ni mali' hii ni istiari inayomaanisha kuwa lazima uishi na utangamane na watu ili uweze kupata mengi kwani watu wana ujuzi tofauti tofauti wa kufaana. Mfano mwingine ni 'Akili ni mali'. Maana ya methali hii, iliyoundwa kwa istiari kulingana na jamii husika ni kuwa akili ya binadamu ni hazina ambayo inaweza kumtajirisha binadamu aitumiapo.

### 2.2.4 Istiari hisimseto

Hii ni istiari ambayo huhamisha hisia za kitu kimoja kwa kingine mfano, **'wimbo ni mwororo'** wimbo umelinganishwa na kitu kinachoweza kugusika na mkono wa binadamu na kuweza kufanya uamuzi kuwa kitu fulani ni laini. Mfano mwingine ni 'Asha ana roho laini'. Hii ina maana kuwa ana roho nzuri yenye upendo na inayojali wengine.

### 2.2.5 Istiari Sahili

Inaeleweka na hadhira kwa wepesi kwa sababu msingi wa kilinganishi na kilinganishwa ni wa moja kwa moja mfano, Asha ni chui. Sifa za chui ambazo ni ukali, wepesi na ujanja zimehamishwa hadi kwa Asha. Hili hufanywa kwa kufana kwa tabia yake. Mfano mwingine ni, Fatuma ni wembe kumaanisha Fatuma ni mkali na husababisha uchungu mkali kwa watu pengine kupitia matusi au vita ama dhuluma nyingine yoyote ile.

### 2.2.6 Istiari radididfu

Hii haiweki wazi msingi wa kilinganishi na kilinganishwa ila hutoa maelezo yanayohusisha au kulinganisha hali mbili.Wamitila (2008:424) anatoa mfano wa istiari hii ambayo ni, "Akihema, alitua na kupiga chenga, akaregesha na kujitoma ulingoni wa siasa." Kuongea kunalinganishwa na kucheza kandanda. Pia wanasiasa wanalinganishwa na wachezaji kandanda.

### 2.2.7 Istiari mseto

Hapa pana kuwa na mfuatano wa istiari kadhaa ambazo zinatumiwa pamoja kurejelea hali moja. Huwa zimetumika istiari zaidi ya moja. Vilinganishi mbalimbali hurejelea kilinganishwa kimoja mfano. Kuhenga ( 1993:6) anatoa mfano huu, "Maisha ya dunia ni bahari, mtu asiyejua kuogelea katika tabu za maisha mwisho hutoswa… maisha ya dunia, mtu sharti awe na dira au ramani…Maisha ya dunia yamelinganishwa na bahari ambayo ni pana, pia ni kama bahari ambayo imejaa misukosuko ndivyo maisha ya dunia yamejaa shida.

### 2.2.8 Istiari changamano

Wamitila (2008 ) anasema ni istiari ambayo hupatikana pale pana istiari kadhaa. Hapa istiari ya kimsingi ambayo ni sahili hutumika kama msingi wa istiari nyingine. Uchangamano unatokea kwa kuwepo kwa vilinganishi kadhaa vya kilinganishi kile kimoja au vilinganishi ama vilinganishwa kadhaa. Kwa mfano neno mvua katika sentensi hii, “ Mvua iliyonyesha nchini baada ya mapigano makali na wakoloni haikuleta mvua ya amani rohoni za wakulima hata baada ya kunyeshewa na mvua hii wakiwa shambani”. Mvua inalinganishwa na maendeleo, utulivu na mapigano mtawalia.

### 2.2.9 Istiari ya dhana

Wamitila (2008) anasema hii ni istiari ambayo hutokea pale ambapo kitu fulani au kitu kilicho katika mawanda maalum kinaeleweka katika muktadha au mwanda mwingine tofauti. Ametoa mifano ‘wakati huruka’ ambao kilinganishi chake’ huruka’ ni ndege ambacho ni kitu thabiti na wakati wenyewe ni wa kidhahania.

## 2.3 Aina za Tashbiha

### 2.3.0 Tashbiha wazi

Maana yake hueleweka moja kwa moja. Uwazi huu hufikiwa kwa matumizi ya kivumishi. Kwa mfano: Kambi ni mjinga kama kondoo. Kivumishi mjinga kimekuwa msingi wa ulinganishi katika tashbiha hii. Kivumishi mjinga huweka wazi tabia / hulka ya kondoo ambayo imehamishwa kwa Kambi.

### 2.3.1 Tashbiha fiche

Tashbiha hii ina ulinganishi fiche. Mhakiki anahitaji kuwaza zaidi kufasiri maana ya tashbiha yenyewe. Anastahili kuwa na uelewa wa hulka na tabia za kilinganishi. Hii hueleweka tu katika kurejelea muktadha wake wa matumizi kwa kuwa kilinganishi kinaweza kuwa na hulka mbali mbali. Tashbiha hii huenda ikaweza kufasiriwa kwa njia mbali mbali kwa mfano, Kei ni nyoka. Neno nyoka lina sifa ya ujanja, hatari kwa kusababisha maangamizi kupitia kinywa na unafiki. Hivyo ni muktadha tu wa matumizi utaweza kusaidia kuelewa ni sifa ipi yatumiwa.

Mfano mwingine ni kuwa, “Yeye hutembea kama tausi”, inaweza kuwa anatembea kwa upole au kwa madaha.

### 2.3.2 Tashbiha ya Kiutendi

Tashbiha hii huwa imefafanuliwa. Wamitila (2003) asema ni tashbiha ambayo hukuzwa na kuendelezwa kwa mapana, huweza hata kufikia mistari ishirini. Asema tashbiha ya aina hii hupatikana sana katika ushairi wa kiutendi. Hata hivyo inaweza kupatikana katika mashairi ya tutumbi. Kutokana na Wamitila tunapata kwamba tashbiha hii huunda taswira inayohusiana na kilinganishi kilichotumiwa. Kwa mfano katika ubeti huu kutoka utendi wa Kalevale kutoka na kitabu cha Knappert (1992).

Akasikia sauti kama ya ndege katiti

ndio sauti ya tunda ikimwita akaenda

Msichana kisikia tunda akakaribia

Na tunda lilimwambia usisite kunijia,

Njoo unile, ni tamu, kunila ndio karamu

Nile sasa,usingoje kabula nyoka asije

Ni tamu kuliko miwa, ni nyeupe, sijaliwa.

Katika ubeti huu, sauti aliyoisikia msichana imefananishwa na ya ndege katiti yaani ilikuwa nzuri mno. Katika uzuri huu sauti imeendelea kumsemesha msichana na kuunda taswira ya usawishi katika maneno haya:

"usisite kuja ,Njoo unile, nile sasa, usingoje".

Hii ni sauti ya tunda (hisia za kujihusisha kimapenzi).

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia msingi wa kinadharia wa taashira, istiari na tashbiha. Chini ya mada hii tumeshughulikia mbinu ya taashira na aina zake maalum. Baadaye tukashughulikia mbinu ya istiari na aina zake huku tukitolea mfano baadhi ya aina za istiari. Mwishowe tukaangazia aina za tashbiha. Katika sura ya tatu tutashugulikia matumizi ya tamathali za semi ambazo ni, istiari, taashira na tashbiha kama zilivyojitokeza katika baadhi diwani ya *Sauti ya Dhiki.*

## SURA YA TATU

### 3.0 Matumizi ya Istiari, Tashbiha na Taashira Katika Sauti ya Dhiki

Ingawa mbinu hizi tatu zimetumiwa katika diwani ya S*auti ya Dhiki*, si mashairi yote yametumia. Kuna mashairi ambayo yana mbinu zote tatu, mengine yana mbili au mojawapo ya hizo tatu kati ya mbinu zingine ambazo hatutashughulikia. Mashairi tuliyochagua tutayashughulikia hapa chini.

### 3.1.0 ISTIARI

#### 3.1.1 N'shishiyelo ni Lilo

Mshairi katika shairi hili anazungumzia imani ya mwandishi kuhusu ukweli aliousema ukamtia matatani kwa kuwekwa kizuizini. Ametumia istiari kadhaa kufikia dhamira yake katika kueleza mambo yaliyomfika baada ya kusema ukweli huu. Kwa mja ukweli ni sumu kwani mja haupendi. Asema:

Kweli n'naifahamu, haipendwi aswilani
Kwa mja hiyo ni sumu, mbaya iso kifani
Mwenye kuitakalamu, hapendezi katwaani
Sasa n'shayaamini, ni kweli haya ni kweli

Ukweli umelinganishwa na sumu. Sumu ni kitu kiangamizacho kikiingia mwili wa binadamu; hata kuua. Hivyo binadamu hupigana na kuambaa sumu yoyote isiwaangamize. Hivyo mja haupendi kamwe ukweli. Mshairi ameng'ang'ana na waja kuhusu ukweli mpaka akatiwa

kizuizini asije akaueneza ukaendelea kuhatarisha maisha ya wakuu wa nchi. Hili ni kwa kuwa wakuu walimwona mbaya kuliko Firauni. Kama ilivyo katika ubeti wanne, mshororo wa tatu:

> Wameniona mbaya, kumshinda Firauni.

Firauni ni istiari yenye maana ya kiongozi wa zamani wa Misri wa kiimla ambaye alikandamiza watu kwa dhuluma kwa kuwapiga, na kuwanyima uhuru wa mapumziko. Hivyo ndivyo mwandishi alivyoonekana na viongozi wa nchi hivyo wakamtia dhikini apate taabu.

Istiari nyingine imetumika katika ubeti wa kumi na sita. Mshairi asema:

> Mateso yao yangawa, nda kuumiza mtima
>
> Hayatakuwa ni dawa, ya kutonipa kusema

Katika mshororo wa pili mateso yalichukuliwa na watesi wake kama dawa ya kuponya au kutibu magonjwa au mambo ya kutetea haki waliyoyachukulia kuwa uovu wa mwandishi. Mwandishi asema mateso hayatakuwa dawa ya kumnyamazisha au kukoma kupigania na kusema ukweli. Dawa imelinganishwa na suluhu ya kumfanya aache kusema ukweli.

### 3.1.2 Jipu

Jipu ni anwani ya shairi na ni istiari kuu katika shairi kwa sababu imetawala shairi hili. Neno hili limetumika katika ubeti wa tatu, sita, tisa na kumi na mbili. Jipu kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004:132) lina maana ya uvimbe mkubwa uliotunga usaha. Jipu huleta uchungu mwingi mwilini mwa binadamu na kusababisha kuhangaika sana. Katika shairi, jipu lina maana ya uchungu unaokera moyoni ambao ulianza siku nyingi zilizopita na unaendelea

kumkera kama jipu (uvimbe) linavyoanza kutunga mwilini na kuendelea kuwa kubwa na kuzidisha uchungu. Mwandishi asema katika ubeti wanne:

Si jana wala si juzi, liliponianza tangu
Ni mingi mno miezi, n'nadhofu hali yangu.

Istiari nyingine ambayo ni kuu ni kipele. Kipele kulingana na TUKI (2004:439) ni upele mdogo na upele ni vituruturu vilivyozagaa katika mwili aghalabu huwasha na kutunga usaha. Katika shairi, kipele hiki kina maana ya matatizo madogo yaliyotokea katika ulingo wa siasa. Mshairi hakuyatilia maanani, mambo aliyaona ni madogo sana kusababisha shida yoyote. Baadaye matatizo haya madogo madogo yaligeuka kuwa makubwa na kumtia kizuizini yaani yakawa jipu. Angejua yatageuka kuwa hivyo angeyaepuka. Angetia dawa. Mwandishi asema haya katika ubeti wa sita:

Kili kipele mwilini, ndiyo mwanzo wake kuwa
Sikujuwa aswilani, kuwa jipu chaja kuwa
Ningekijuwa zamani, ningekitangiya dawa.
Nikwamba sikutambua, ndipo hakiwatiliya

Katika ubeti huu wa sita, istiari nyingine ni dawa ambayo ina maana ya suluhu ya matatizo yale madogo madogo.

### 3.1.3 Mamba

Shairi hili lina istiari "mamba". Neno hili lina maana ya mnyama hatari wa majini ambaye hula wanyama wengine kama chakula chake. Mamba hutumia njia mbalimbali kuwala wanyama

hawa. Huwameza  wakiwa hai au kuwauwa kwanza kabla ya kuwala. Wanyama wengine huuliwa wanapofika mtoni kuyanywa maji, ili kukata kiu na waendelee kuishi. Maana ya istiari hii ni kiongozi wa nchi ambaye anajigamba na kujiona hodari kwa kuweza kuangamiza na kutumia nguvu zake kupata chochote atakacho kama mamba. Mshairi asema afikiri hataishiwa na nguvu na ataishi milele yaani uongozi wake hauna mwisho. Mwandishi anena katika ubeti wa pili:

Kuna mamba ,mtoni metakabari

Ajigamba, na kujiona hodari

Yuwaamba, kwamba ’taishi dahari

Huyu mamba (kiongozi) aishi mahali ambapo mwandishi apataja kwa jina mtoni.  Mtoni ni istiari. Ni mahali ambapo wanyama wengi wa aina aina waishi. Mtoni kumelinganishwa na nchi ambapo watu wa aina aina au wenye mitazamo tofauti tofauti huishi.

### 3.1.4 Ukamilifu wa Mja

Mshairi, katika shairi hili, amezungumzia kuhusu ukamilifu wa mja akitumia istiari ya viungo vya mwili kurejelea binadamu. Katika ubeti wa kwanza ametumia maguu. Anasema mtu kuwa na maguu si kwamba amekamilika. Maguu humpa binadamu uwezo wa kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kuweza kutembea hakumpi binadamu yale yote mahitaji anahitaji hivyo maguu ni sehemu tu ya mahitaji ya binadamu bali si kila kitu kwake.

Katika ubeti wa pili, msanii ametumia istiari ya tumbo. Asema:

Mtu kuwa na tumbo, si kwamba mekamilika

Tumbo ni kiungo cha mwili kinachowezesha binadamu kupata nguvu baada ya kuweka chakula kikasagwa na kuwezesha kusafirishwa mwilini kwa viungo vingine. Kama binadamu angekuwa na tumbo pekee liwekwe chakula pengine kisagwe haingesaidia kwani hakingeweza kufikia sehemu zingine za mwili bila usaidizi wa viungo vingine. Pia binadamu kuwa na tumbo inaweza kumaanisha binadamu ana mahitaji mengi zaidi ya tumbo.

Kuna istiari nyingine katika ubeti wa tatu mshororo wanne ambayo ni kifua. Mshairi wasema:

Mtu kuwa na kifuwa, si kwamba mekamilika

Kifua huwa kimesheheni viungo vya maana zaidi kama moyo ambao hutumika kuwezesha damu kufikia kila kiungo cha mwili na hivyo binadamu huwa hai na mwenye nguvu. Ingawa aweza kutumia kifua au nguvu hizi apate hiki au kile, hili halitoshi; bado binadamu hajakamilika. Hata akiwa mwenye nguvu kupindukia huenda akapata pingamizi zilizozidi nguvu zake.

Mbali na hayo, binadamu huweza kuwa na maungo. Maungo ni istiari inayosimamia hulka ya nje ya mtu, yaani binadamu amekua na akionekana ni mzima kutoka nje. Yaani anaoneka kama kwamba hajakosa lolote. Hata hivyo, haya hayatoshi kwani daima binadamu akipata hiki ataka kile. Maungo vilevile huwa na maana ya nguvu za mwili. Nguvu hizi humwezesha binadamu kutenda kazi ya sulubu au kupigana vita hasi na chanya. Kwa mfano, huweza kumpiga mtu ili kumhasiri na kumharibu sura au kumpigania na kumwokoa kutoka dhuluma za kivita. Binadamu afanyapo kazi za sulubu huweza kusaidia katika uzalishaji wa baadhi ya mali katika nchi. Hata hivyo, haya hayatoshi. Binadamu huhitaji zaidi ili kukamilika.

Kiungo kingine cha mwili ambacho mshairi ametumia ni mikono. Hii ni istiari yenye maana ya kufanya au kiungo cha kutenda. Kutenda kwa mikono tu hakutoshi. Mikono inaweza kusaidia binadamu kuandika amri au ujumbe wowote ule lakini hauwezi fikia wengine kwa kuwa umeandikwa. Mkono huweza kutia chakula mdomoni binadamu ale, lakini chakula hiki kinahitaji kuwa kimefikishwa kwake aweze kula. Kiungo kingine ni shingo ambayo hutumika kushikilia kichwa, kuunganisha kichwa na sehemu zingine za mwili. Bila shingo, umoja huu hauwezi kuwepo. Shingo ni kiwakilishi cha binadamu wanaopatanisha wengine katika jamii. Wao hupatanisha mafidhuli na wenye kauli ambazo hazina mwelekeo, kama asemavyo mshairi

" na kuna wenye kauli, zisokuwa na ushingo" pia "kuna vipofu na wenye chongo". Hawa huweza kupewa upatanisho na watu walio kama shingo ili waweze kupata mwelekeo. Hata hivyo kuletwa pamoja na kupata mwelekeo hakutoshi.

Mshairi asema, katika ubeti wa saba, kuwa kiungo kidevu ingawa binadamu huwa nacho si kwamba amekamilika. Kidevu ni sehemu ya chini ya uso ambayo hupa uso sura nzuri ya katika sehemu ya chini.Hata hivyo haijaleta ukamilifu kwa mja. Hawa ni watu katika jamii ambao huleta urembo na ukamilifu wa sehemu za maisha ya binadamu. Ni wenye heshima, huruma na wema. Mambo haya tu humkamilisha mja au jamii kwa sababu kuna wengine katika jamii ambao ni waovu, wenye adabu mbovu na wanaotenga nguvu kama mshairi anavyosema katika ubeti wa saba. Ili uso kukamilisha urembo wake na kazi yake unahitaji mdomo, meno, ulimi, pua, masikio na macho.

Mdomo, meno, ulimi, pua, masikio na macho ni istiari zilizo katika ubeti wa nane hadi wa kumi na tatu. Mdomo hutumika kusema. Hiki ni kiwakilishi cha watu katika jamii ambao husema au

huwa na sauti na jamii huwasikiliza. Sauti hii hukashifu, husifu au huweza kufanya uchochezi watu wakatengana. Hivyo sauti pekee haitoshi. Pia ulimi hutenda kitendo kiki hiki ukiwa na mdomo.

Ulimi na mdomo vikisema vinahitaji binadamu anayepumua kupitia pua. Pua hupitisha hewa mwilini ili kila kiungo kiwe hai. Hawa ni watu wakarimu katika jamii wanaotenda haki. Na kuna madhalimu walio hai wanaonyima watu haki. Hivyo, binadamu kuwa apumua hakutoshi.Ahitaji mengine akamilike.

Binadamu huwa na kichwa kinachomsaidia kufikiri hivyo kuwa na tabia njema. Hata hivyo, kuna watu wenye kichwa lakini mshairi asema katika ubeti wa kumi na nne, mshororo wa tatu katika utao:

**“**Hino hawanayo katwa”

“Hino” ikiwa na maana ya tabia njema. Hivyo kichwa pekee huwa hakitoshi binadamu kuwa nacho.

Katika shairi zima kuna istiari za viungo vya mwili ambavyo vinamwakilisha binadamu. Hili huenda likawa na maana kuwa binadamu huhitaji kushirikiana na wengine, ili aweze kufanya kazi kikamilifu, kwani hakuna binadamu anayeweza kutenda yote.

### 3.1.5 Mnazi: Vuta n’kuvute

Shairi hili ni ngojera. Alii na Badi wanawasiliana. Mshairi ametumia istiari katika mazungumzo yao. Kwa mfano katika ubeti wa kwanza, Alii asema:

" Ndugu ulo mnazini, wanitafuta balaa

Nakwambiya shuka tini, katakata wakataa

Utashuka au la?

Istiari katika ubeti huu ni mnazi umelinganishwa na uongozi. Mnazi ni mti wenye manufaa makubwa katika mwambao wa pwani. Yeyote apandaye mnazi huwa na nafasi ya kuchuma nazi na kunufaika kwayo. Maana nyingine ya "mnazi" ni nchi ambayo inastahili kunufaisha kila mwananchi. Nchi inapotawaliwa na wachache yaani kuifanya maskani wengine walioachwa nje hutaabika.Istiari nyingine ni:

'Kufanya ni maskani'

Istiari hii ina maana kuwa walio uongozini wamefanya nchi kuwa yao. Maskani ni mahali pa mtu binafsi na hulinda na kufanya lile la kumfurahisha akiwa huko. Hii ni kwa sababu ni miliki yake. "Nazi" ni neno lenye maana ya "matunda yanayozaliwa na mnazi". Neno hili (nazi) limetumiwa kama istiari likilinganishwa na matokeo ya maendeleo ya nchi. Alii alisema anataka kukwea mnazi ili atunde nazi yaani ayafurahiye matunda ya uongozi. Pia ina maana ya kuwa anataka kutumia mali ya nchi kama vile viongozi wanavyofurahia. Alii asema katika ubeti wa tatu:

Sababu ya kukwambiya, ya kwamba ushuke tini

Ni kuwa nataka kweya,huko juu mnazini

Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani

N'shakueleza kwa nini.

Jambo hili la kukwea atunde nazi limerudiwa katika ubeti wa kumi na tano.Nazi katika ubeti huu imelinganishwa na mali ya nchi au matunda ya maendeleo ya nchi.

Maneno ’wangu wana’ katika ubeti wa arubaini na tatu ni istiari yenye maana ya wafuasi wa chama cha mshairi. Hawa (wangu wana) ni wale wana maoni na mtazamo sawa na mshairi ambao wamedhulumiwa kwa muda mrefu bila kusema lolote kama asemavyo mshairi katika mishororo hii:

Siku ikitwa hatuwa ,pamoja na wangu wana
Pasiwepo na kunena.

**3.1.6 Telezi**

Mshairi ametumia istiari katika shairi hili kuficha ukweli. Kwanza kabisa anwani ya shairi hili ni ya kiistiari. Anwani (telezi) imetokana na kitenzi “teleza” ambacho kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004:401) kina maana ya kuserereka kama mtu anapokanyaga mahali penye tope au palipo poroja. Pia ina maana kung’ang’ana. Maana ya telezi ni hii hali ya kung’ang’ana au kuserereka kwa sababu ya matope. Katika shairi zima hali ya telezi ya mimea, na kazi ngumu waliofanya wakulima imetendeka hivi kwamba hakuna kilichomnufaisha mwananchi (mkulima).Mshairi asema hili katika ubeti wa pili:

Mimeya walioipanda, ilitekukatekuka
Kazi ngumu walotenda,yote ikiharibika
Hawakuvuna matunda,waliyo wakiyataka
Waliyo wakiyataka,yakawa ya mbali nao**.**

Katika ubeti huu, mshairi amaanisha kila walichotenda kilipata utelezi na kuwaponyoka. Hawakupata faida yoyote.Telezi ni pingamizi za viongozi.

Istiari nyingine ni ulinganisho wa ngurumo na maradi na juhudi nyingi walizotia wananchi. Kutokana na juhudi hizi kukawa na maendeleo makubwa ambayo yamelinganishwa na mvua hii iliyonyesha kutwa na kucha kukesha. Yaani usiku na mchana matokeo ya juhudi za wananchi yalionekana lakini hayakuwafaidi kwani mshairi katika ubeti wa saba mshororo wa kwanza asema:

Zikanibwaga telezi , sikujuwa kuzendeya.

Haya matokeo yalikuwa tope ambazo huleta telezi yenye maana ya mambo yanayowafanya wananchi kuanguka wasiende mbele au kuanguka wakaumia na kuchafuka; wanashindwa kutembea matopeni.Tope pia ni istiari yenye maana ya kule kufungwa kwa mshairi asiende mbele wala nyuma. Akiri katika ubeti wa sita:

Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndoana

Kujaribu kwenda mbele ingawa kwa dhiki kwa mshairi kukawa ni mfano wa samaki kuiendeya ndoana yaani kufungwa.

Ndoana ni istiari nyingine ambayo ni ulinganisho na jela au ngome.Katika ubeti wa saba mshairi ametumia kitenzi “kutembeya” kikiwa istiari yenye maana ya kupigania haki.Asema ni mwendo tu atabadilisha katika mshororo huu.

Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo.

Telezi ni istiari yenye maana ya makosa aliyoyafanya mshairi yaliyomtia matatani badaaye na kumsababishia majuto ya msimamo mkali aliouchukua.Haya anayakiri katika ubeti wa saba:

Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi, yazingenifika haya
Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo

### 3.1.7 Semeni  Wenye Kusema

Katika shairi hili mshairi ametumia mbinu za tamathali za semi ili kuremba kazi. Ametumia istiari katika kibwagizo, anasema:

Musijifanye migombe, semeni wenye kusema.

Istiari hapa ni neno “migombe”, ambalo ni ng’ombe wakubwa na wengi. Ng’ombe hapa ana sifa ya ujinga. Hivyo mshairi anawauliza wenye kusema wasijifanye wajinga (migombe) waseme.

Mshairi ametumia istiari nyingine katika ubeti wa sita anapotumia neno simba, anasema:

Na wale waliyo simba,leo wangurume ujumbe.

“Simba” ni mnyama mkali na ambaye huogopwa na wengi porini.Hii ina maana kusema kwa ukali ili watu waogope kwa ukali wao.Watu wanaorejelewa kama simba ni viongozi wenye uwezo mkuu.

### 3.1.8 Muwerevu Hajinyowi

Mshairi ameiremba kazi hii na kufikisha ujumbe kwa njia fiche kwa kutumia istiari.Katika ubeti wa kwanza ametumia istiari "ngoma" kwa maana ya "utajiri" na "nguvu za povu" kuwa na maana ya kitu "dhaifu". Povu ni viputoputo vya hewa vinavyotokea juu ya kitu majimaji, aghalabu kwa kukorogwa. Povu halidumu huisha haraka. Hivyo utajiri huu unaomfanya anayerejelewa katika shairi kuuliza kama utajiri wake utakesha au kudumu ama ni kitu dhaifu tu. Mshairi auliza hili katika mshororo wa tatu katika ubeti wa kwanza:

Ngoma yako itakesha au ni nguvu za povu?

Istiari nyingine imetokea katika ubeti wa pili mshororo wa tatu:

Wafikiri kisu gutu,hakikati nyama pevu?

Istiari, "kisu gutu" ina maana ya kisu ambacho hakina makali. Kisu hiki kinalinganishwa na mtu asiyejielewa. Nayo istiari "nyama pevu" ni ulinganisho wa mtu mwenye ujuzi au aliyekomaa. Katika ubeti wa mwisho, yaani wa tano, mshairi ametumia maneno "mbiti na mbivu", kama istiari kumaanisha "mambo maovu" na "wema" mtawalia.

Katika ubeti wa nne mshororo wa tatu mshairi asema:

Iko siku itajiri, ujikute kwenye wavu**.**

Hapa ametumia "wavu" kama istiari. "Kuwa kwenye wavu" ni ulinganisho wa "kushikwa na kutoweza kutenda utakalo kwa kuwa mhitaji". Kuwa katika wavu ni kuwa katika hali ya kutojiweza. Hivi ndivyo itakavyokuwa siku moja kwa wale werevu.

### 3.1.9 Ah! Mwenzangu

Mshairi ametumia istiari anapotumia neno “pweza”. “Pweza” kwa mujibu wa TUKI (2004:344) ni mnyama wa baharini mwenye umbo la duara liliozungukwa na mikono au minyiri minene. Kwa mikono yake minene hufanya vurugu huko baharini anamokaa.Naye mshairi katika shairi amelinganishwa na pweza kwa sababu ya tabia yake ya kusababisha vurugu na kujitia matatani mwenyewe.Katika ubeti wa kwanza mshororo wa mwisho mshairi asema:

Ufanyayo ni ya pweza,kujipaliya makaa

Katika ubeti wa pili, mshororo wa tatu, mshairi ateta kwa vurugu za mwenzake. Anasema:

Huwa wanipa matungu, utendapo jambo baya.

Istiari nyingine zimetumika katika ubeti wa tano. Neno “ngoma” limetumika kama istiari kulinganisha na jinsi matendo ya mhusika au mwenzake mshairi ambayo yamefurahisha ayatendapo.Hivyo ni kama ngoma. Ngoma huchezwa na watu wanapokuwa na furaha. Mwandishi anasema:

Imekufurahisha ngoma,mshipani mekungiya

Haya matendo yamelinganishwa na “donge la sukari” ambalo ni tamu na ambalo mwenzake mshairi amelibugiya. Mshairi asema katika ubeti wa saba:

Donge la sukari tamu,ambalo melibugiya.

Katika mshororo huu “kulibugiya donge la sukari” kunalinganishwa na “kuwatesa wenzake”.Yaani amejitolea kuwatesa wenzake.Hiki kitendo “kubugia” ni istiari. Pia kuna istiari “sumu” ambayo ni ulinganisho wa maovu. Mshairi anasema:

Kati yake muna sumu, kama hujuwi sikiya.

Hapa anamaanisha kati ya mambo ayatendayo mhusika (mrejelewa) mengine ni maovu na ni hatari kama ilivyo sumu.

**3.1.10 Mamaetu Afrika**

Katika shairi hili, mama ni jina ambalo limetumika kiistiari. Afrika imelinganishwa na mama. Mama huwatunza watoto kwa njia kama vile kuwapa chakula, kuwafulia, kuwafariji na kuwafunza adabu maishani. Pia kuwapa watoto matumaini. Hivi ndivyo bara la Afrika huwafanyia (kushughulikia mahitaji) watu waliyo wenyeji wa bara hili. Hata, hivyo msanii asema kuwa mali ya mama imechukuliwa (kutawaliwa) na mama amedhulumiwa.Yaani bara la Afrika kutendewa maovu. Mama ni istiari kuu;imetawala shairi.

Istiari nyingi zimetumika katika ubeti wa pili:

Si watu hawa,ni wanyama wa mwituni

Hapa wakoloni wamelinganishwa na wanyama wa mwituni.Wamelinganishwa na wanyama, kwa sababu ya ukosefu wa huruma, kutowafikiria wengine na kutendea Mwafrika unyama kwa kupokonya Afrika mali kama asemavyo mshairi katika ubeti mshororo wa nne:

Mali nyingi ya thamani,wakakupokonya Mama

“Manyani” ni jina la wanyama wa mwituni na limetumiwa kama istiari. Wanyama hawa wanalinganishwa na waafrika na mkoloni kwa sababu ya kumkosea heshima Mwafrika kwa weusi na utu wake. Mshairi asema katika ubeti wa saba:

Hawakuthamini utu, wa walo na ngozi hini.

Wakituona manyani, kwamba tu weusi Mama.

Istiari nyingine ni “dawa”. Dawa imetumiwa kwa maana ya suluhisho ambalo wakoloni walipata kuhusu ufahamu wa umoja wa waafrika ambalo ni kuwatenganisha. Mshairi asema katika ubeti wa kumi na tano:

Hapa wakakatikiwa, kwamba watutenganishe

Kwani wamoja tukiwa, tutawakanyanga weshe

Wakaona kubwa dawa, wano watutenganishe

Ili wakukorofishe, na kukunyonya we Mama

“Dawa” pia limetumika katika ubeti thelathini na moja kwa ulinganisho huu huu.

Katika ubeti ulio hapa juu, wa kumi na tano, mshairi ametumia neno “kunyonya” kama istiari yenye ulinganisho wa kutumia vibaya mali ya Afrika. Neno lingine ambalo limetumiwa kiistiari ni mbwa. Mbwa limelinganishwa na mkoloni ambaye alikuwa amepata fupa (Afrika) lakini ameacha kuliguguna. “Kuguguna” ni istiari pia yenye maana ya kufaidika na mali ya Afrika. Mshairi asema katika mshororo huu ubeti wa ishirini na saba.

Ni mbwa kuona fupa, akacha guguna Mama

### 3.1.11 Jana na Leo na Kesho.

Katika shairi hili mtunzi anazungumzia mambo yaliotendeka, yanayotendeka na yatakayotendeka. Mshairi ametumia istiari kwa mfano neno “jana”. Jana katika shairi hufananishwa na mambo yaliyopita. Ndio maana mshairi asema katika ubeti wa nane:

> Jana ni ya kukumbuka,vitendo viliyopita.

Istiari “jana” ni istiari kuu kwani imetawala shairi.Neno hili limetajwa katika beti nyingi kama ubeti wa, kwanza, pili, nne, sita, saba, nane, tisa, kumi na moja na ishirini na sita. Neno lingine ambalo ni istiari ni “marehemu”. Mshairi asema katika ubeti wa saba:

> Ya jana hufa na jana, yakawa ni marehemu

Hapa neno “marehemu” limetumiwa likilinganishwa na jana ambayo ikipita hairudi. Imekuwa mfu, haiwezi kuwa hai tena.Yaani mambo ambayo yamepita ni kama binadamu aliyekufa ambaye haonekani tena duniani.

Istiari nyingine ni “leo” ambalo ni neno linalorejelea au kusimamia nyakati tunazoishi sasa. Nyakati ambazo tuna uwezo wa kufanaya kazi. Hili linatokea mshairi asemapo kuwa leo ikija ipokewe na kupewa maneno mema kwani huenda ikampa binadamu mazuri ( mshairi ayaita manono manono). Pia asema tuwe waangalifu isituponyoke, tusije tukajuta. Hivyo, “leo” ni istiari inayolinganishwa na nyakati za uwezo wa kufanya kazi pengine ujana na makamo.

Kesho ni kiwakilishi cha mambo yanayokuja , mshairi anasema katika ubeti wa ishirini:

> Kesho mithili ya mwana, aliyemo matumboni
>
> Hujuwi ni mvulana, msichana au nini

Au kama atapona, ajapo ulimwenguni

Huwa hunayo yakini

Mshairi asema kesho haijulikani itakavyokuwa. Mambo yajayo hayana yakini. Hayajulikani kama yatanyooka au la. Ni kama kilinge tumboni.

Katika ubeti wa kumi na mbili mshairi ametumia maneno “manono manono” ambayo ni istiari yenye maana ya “mambo mazuri”. Mambo mazuri yanalinganishwa na mambo manono manono. Mshairi asema:

Hwenda ikakukidhiya, yalo manono manono

**3.1.12 Usiniuwe**

Shairi hili linazungumzia kuhusu mama na kilinge wakizungumza. “Mama” na “kijusi” ni istiari yenye ulinganisho wa vyama vya kisiasa ambavyo vinapigania nafasi. Kwa mujibu wa Chacha (1992) nchi ya Kenya ilipopata uhuru kulikuwa na vyama viwili KANU na KADU, ambavyo viliungana na kuunda serikali chini ya chama cha KANU. Makamu wa rais akahisi kwamba ametengwa na kuunda chama kipya (Kenya Peoples Union). Chama hiki cha naibu wa rais wakati huo ndicho kinalinganishwa na kilinge kinachoongea katika shairi. Mama analinganishwa na kile chama cha KANU kinachotawala. Chama kipya cha KPU kinaomba kupewa nafasi kijitafutie wafuasi na mamake KANU. Mshairi asema katika ubeti wa kumi na tisa mshororo wa kwanza na wa pili:

Sikosi wa kunitwaa, aniswafishe ujusi

Niliyapo ng’aa ng’aa! Aniongowe upesi

Istiari nyingine ni “pande la damu” katika ubeti wa tisa na “nofu la nyama” katika ubeti wa kumi. Istiari hizi mbili, “pande  la damu” na “nofu la nyama” , ndio maneno yanayolinganishwa na “kukua na kunawiri” kwa kupata nguvu kwa chama kipya cha KPU; kumelinganishwa na hatua za kijusi kukua.

Mfano mwingine ni “uhai” ambao ni kilinganishi cha haki ya chama kuwepo. Mshairi asema katika ubeti wa kumi na moja mshororro wa tatu:

Hana hakika kunipoka, uhai ni haki yangu

KPU kiliambia serikali kuwa kina haki ya kuwepo. Hivyo kikaomba mama, serikali (chama tawala) ikihurumiye.  Pia katika ubeti wa kumi na mbili kuvunja chama kunalinganishwa na kuua. Mshairi asema katika ubeti wa kumi na mbili na ishirini na sita mtawalia:

Huna haki kuniuwa , japo sijakamilika

Mama wata kuniuwa, mamangu nihurumiya

Istiari nyingine ni “mlimwengu” .Wafuasi wamelinganishwa na mlimwengu ambao  mshairi asema  hawezi kuwakosa katika ubeti wa kumi na nane;

Sitakosa mlimwengu, ambaye atanilea

Mlimwengu ni wafuasi wa chama na wafadhili ambao watalea chama.

Katika ubeti wa ishirini na mbili, mshairi ametumia istiari “kujipinda”. Kujipinda kumelinganishwa na kung’ang’ana mpaka mambo yawe sawasawa, kama mshairi anavyosema katika mshororo huu wa pili;

Sitawata kujipinda, kwamba sawasawa yawe

### 3.1.13 Mambo Yana Mambo Yake

Mshairi anagusia mambo yanayohitajika ili mambo yote yanyooke; yaani kila kitu kitendeke vyema. Mshairi ametumia istiari kama:

Mambo ni mteremko (ubeti wa saba)

Hapa mshairi asema pasiwe na mtu wa kufikiria kuwa mambo ni mteremko. 'Mambo ni mteremko' ni istiari inayolinganisha urahisi wa mambo na mteremko.

### 3.1.14 Watiliye Pamba

Kutilia pamba ni kufunga masikio usisikie lolote. Mshairi ametumia istiari katika ubeti wa tatu mshororo wa tatu asema:

Wa mbiyo mafundi, tuwe mbali mbali

Neno "mafundi" ni istiari ambayo inalinganishwa na watu wanaojenga utengano kati ya watu wawili wapendanao ambao ni mshairi na mwenzake.

### 3.1.15 Wasafiri Tuamkeni

Katika shairi hili, mshairi anahimiza wananchi wainuke waendelee na safari yaani kupigania haki zao. Neno "safari" ni istiari kuu, kwani neno hili limerudiwarudiwa katika kila ubeti. Neno "safari" limelinganishwa na mapigano ya kisiasa ambayo si rahisi kwani njiani 'kuna miba yenye sumu', kama anavyosema mwandishi.

Istiari nyingine ni “nyama mwitu”. Wanyama wa mwitu wamelinganishwa na wapinzani wa kisiasa ambao ni wadhalimu kwa mshairi na wenzake. Wapinzani hawa wamelinganishwa na miiba yenye sumu. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

Kuna miiba yenye sumu, tunzani tusidungike

Istiari katika mshororo ulio hapo juu ni “miiba yenye sumu”. Wapinzani wa mshairi na wenzake ni hatari mno; wanaweza kuwaangamiza wasipojitahadhari.

Katika ubeti wa kumi mshairi auliza wasafiri waingie mistarini na kujipanga safu safu. Katika mshororo wa pili asema:

Ngiyani misitarini, safu safu mupangike

Istiari ni “kuingia mistarini” ambayo imelinganishwa na kuchukua mtazamo wa mshairi na wenzake au wasafiri na “safu safu” ni istiari ambayo imelinganishwa na kuwa na usawa kifalsafa.

Neno lingine ambalo ni istiari ni “maguu”. Kuwa na uwezo wa kupigana kunalinganishwa na kuwa na maguu ambayo yananyosheka. Mshairi asema katika ubeti wa kumi na moja mshororo wa pili:

Wale walio wazima, maguu nayanyosheke

Kunyosheka kwa maguu ni kutumia uwezo wa wasafiri kujipanga na kufuata.

### 3.1.16 La Mjini na La Shamba

Shairi hili lina anwani ambayo imeegemea methali 'jogoo wa shamba hawiki mjini' kama mshairi anavyouliza katika mshororo wa mwisho ubeti wa kwanza. Mshairi ametumia istiari katika ubeti wa pili anaposema:

Usibaranganye mambo, simba awapo, ni simba

"Simba" ni mnyama ambaye mwandishi amelinganisha na "kiongozi mwenye nguvu" na akiwepo pasiwe wakujidanganya kuwa hawezi kutenda mambo kwa uwezo wake mkuu.

Istiari nyingine ni 'jimbi la shamba na la mjini'. Hawa majimbi wametumiwa wakilinganishwa na "viongozi wawili". Jimbi wa shamba ni kiongozi ambaye hana uwezo mkuu na mpevu kimawazo kama yule wa mjini. Hivyo kila kiongozi astahili kuhifadhi sehemu yake. Wa nafasi ya juu aihifadhi (jogoo wa mjini) na awike huko. Yule wa nafasi ya chini (jogoo wa shamba) akae pale pale na awikie nafasi iyo hiyo.

### 3.1.17 Ndiya Panda

TUKI (2004:310) asema njia panda ni makutano ya barabara. Katika shairi "ndiya panda" ni istiari yenye kulinganishwa na "kutoweza kufanya uamuzi" kuhusu jambo. Istiari nyingine ni neno "safari". Neno hili linalinganishwa na "mambo atakayotenda" mshairi. Asema katika ubeti wa kwanza, sita, tisa na kumi na sita:

| | |
|---|---|
| Ubeti wa kwanza: | Safari naloiyanza, bado ningalimo kwenda |
| Ubeti wa sita: | Pamwe kuchoka hiyau, safari sikuivunda |
| Ubeti wa tisa: | Ilipofika safari; silijuwi la kutenda |
| Ubeti wa kumi na sita: | Nipani la muwangaza, safari 'sije ivunda |

Katika mishororo hii ambayo imetoka beti tofauti neno safari linarejelea mambo atakayotenda ambayo aliyaanza katika ubeti wa kwanza na katika ubeti wa sita asema kuwa juu ya kuchoka bado ataendelea mambo haya yasiharibike. Hata hivyo katika ubeti wa tisa asema ifikapo safari yaani ilipokuwa ni kuanza kuyatenda mambo hakujua la kufanya. Hivyo katika ubeti wa kumi na sita aomba kupewa mwangaza mambo (safari) yasiharibike.

### 3.1.18 Kichu Hakiwi ni Uchu

Anwani ya shairi hili yaeleza kuwa kitu hakina thamani lakini kilicho na thamani ni utu. Haya ndiyo mshairi azungumzia akitumia tamathali mbalimbali za semi. Hapa sisi tunashughulikia istiari. Mshairi ameitumia katika ubeti wa thelathini na nne. Asema:

Badili hiyo furusa, kuitumiya vizuri
Kwake sivyo; bali sasa, huanzisha takaburi
Wende awe kuwatesa, awatendee jeuri
Huyo ni mnyama pori, hafai kuitwa mtu

Mshairi amelinganisha mtu anayetumia cheo chake kuwadhulumu wengine na "mnyama wa pori".

### 3.1.19 Zindukani

Mshairi awaambia watu wenye kujigamba na kujitakia makuu wazinduke. Akiwaambia hili atumia tamathali za semi kama vile istiari. Katika ubeti wa kwanza mshairi ametumia neno "dawa". Neno hili lalinganishwa na "suluhu" ya mambo yanayomsumbua mshairi na wenzake.

### 3.2.0 TAASHIRA

Ingawa Abdilatif (1973) ametumia mbinu ya taashira katika mashairi yake katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*, hata hivyo si mashairi yote ambayo yameitumia tamathali hii. Kati ya mashairi ishirini ambayo tulihakiki haya yalioko hapa chini ndiyo yametumia mbinu hii.

### 3.2.1 Jipu

Mshairi anazungumza kuhusu dhuluma alizopata msanii kizuizini. Aliliita shairi lake "Jipu" ambayo ni taashira inayorejelea "dhuluma" hizi. Ametumia tamathali taashira nyingine katika ubeti wa tisa aliposema kuwa atalifinya jipu hadi litumbuke. Huku "kuliminya" ni ishara ya "kupigana" na "kutumbuka" ni ishara ya "kushinda". Hivyo mshairi atapigana hadi apate uhuru. Katika ubeti wa kumi na mbili mshairi asema baadaye jipu litabaki kovu mwilini. "Kovu" ni ishara ya "kumbukumbu ya mateso" aliyopata mshairi katika harakati za kujikomboa.

### 3.2.2 Mnazi: Vuta N' Kuvute

Mshairi ametumia neno "chombo" likiwa ni ishara ya "nchi". Mshairi asema katika ubeti wa thelathini na mbili mshororo wa tatu:

> Chombo kitakapozama, na kuzama walo ndani

Mshairi anamaanisha chombo ambacho ni nchi itakapozama au kuangamia, itaangamia pamoja na wananchi.

### 3.2.3 Telezi

Mshairi ametumia taashira katika ubeti wa nne. Asemapo:

Na mijaji kwa mikondo, yakawa barabarani

Yakawa barabarani, mvua kwisha kunyesha

"Mijaji kwa mikondo" ni ishara ambayo ni ulinganisho wa "ushahidi" kwamba maendeleo kwa kweli yalikuwa yametendeka kama vile maji yanavyopita barabarani baada ya mvua kunyesha. "Mvua" iliyonyesha ni ishara ya "rasimali" ilioko katika nchi. Hivyo mvua ni taashira ya mambo ya kimsingi ambayo huhitajika kuleta maendeleo katika nchi.

**3.2.4 Mamaetu Afrika**

Mshairi anazungumza kuhusu bara la Afrika. Ametumia tamathali ya taashira asemapo katika ubeti wa kumi;

Ndiyo yaliyowalisha, na kutengeneya huko

Miji wakasimamisha, kwa nguvu za mali yako

Lililowatajirisha, ni jasho la mwili wako

Na damu ya wana wako, ndiyo kuwa hayo

Neno "damu" na "jasho" ni vitu ambavyo ni sehemu ya binadamu ambayo inamrejelea binadamu mwenyewe. Hii ni kwa sababu si damu wala jasho tu zilitumika bali binadamu; kila sehemu ya mwili wake ilitumika. "Damu" na "jasho" ni vilinganishi vya "nguvu" na "bidii" ya binadamu.

**3.2.5 Usiniuwe!**

Katika shairi hili mshairi ametumia taashira kadhaa. Kwa mfano katika ubeti wa nane

Ni manii tone moja, la maji madhalilifu
Tone lililojituja, kutoka maji machafu
Ndicho chanzo changu kuja, nabado ndiya ni ndefu
S'anze sasa kunifuja, mamangu nihurumiya

Taashira ni "manii tone moja". Hili 'tone" ni ishara ya "wazo" ambalo lilileta tofauti katika vyama na kuzua michafuko kati yao. Manii tone moja ni chanzo cha kilinge kutungwa yaani ndicho chanzo cha chama kipya cha K.P.U kuundwa. Neno tone katika ubeti wa tisa lina maana ya hilo wazo.

Taashira nyingine imetumika katika beti kadhaa mshairi anapotumia neno "tumbo" na "tumboni'. Hapa ni mahali ambapo mtoto hukulia na chama cha K.P.U kilikuwa ndani ya "KANU" ambacho ndicho tumbo au tumboni. K.P.U chaomba kutopigwa marufuku hata kabla hakijajitenga na chama tawala. Katika ubeti wa kumi na tisa mshairi asema:

Niliyapo ng'aa ng'aa! Aniongowe upesi

"Kulia ng'aa ng'aa" ni ishara au taashira yenye maana ya "kuzaliwa au chama kuundwa". "Kuongowa upesi" ni taashira nyingine yenye maana ya "kupata wafuasi mara moja" wakuendeleza. Nacho kitendo cha "kuua" ni ishara ya "kukinyima chama nafasi" ya kujiendeleza.

### 3.2.6 Mambo Yana Mambo Yake

Mshairi ametumia taashira 'jasho kutona' ikiwa ni ishara ya "kufanya kazi kwa bidii". Pia "kunyoshwa viungo" ambako kuna maana ii hii ya "kufanya kazi".

### 3.2.7 Watiliye Pamba

Shairi hili limetumia taashira moja pekee ambayo ni 'kutilia pamba'. Kutia pamba masikioni kumelinganishwa na "kutosikiliza".

### 3.2.8 Wasafiri Tuamkeni

Katika shairi hili neno "bendera" ni taashira. Ni ishara ya "uhuru". Neno hili limetumika katika ubeti wa pili na wa saba ikiwa na maana hii ya uhuru. Katika ubeti wa kumi na tatu neno hili limeunganishwa na lingine likawa "mshika bendera" likawa na maana ya "viongozi".

### 3.2.9 Ndiya Panda

Mshairi ametumia taashira 'ndiya panda'. Ishara hii ina maana ya "kutojua pakuelekea" au "kushindwa kufanya maamuzi". Maneno haya 'ndiya panda' yamerudiwa katika kila ubeti. Taashira nyingine ni "mawe" ambayo huwakilisha "ugumu". Mawe ni ishara ya "wapinzani" wake mshairi ambao ni hatari na wakatili. Mshairi anasema hili katika ubeti wa kumi na nne:

> Ni kama ni'loangama, na kushuka kwanishinda
> Na hata lau nasema, nijitupe kama bunda
> Sitaanguka salama, kwenye mawe tajidunda.

### 3.2.10 Kichu Hakiwi ni Uchu

Mshairi ametumia taashira ambayo ni neno “ndovu” katika shairi hili. “Ndovu” ni ishara ya “ukubwa” na “uwezo mkuu” na katika shairi ni binadamu ambaye huwa na mali na uwezo mkuu lakini huwadhulumu watu. Hivyo anakuwa kama mnyama ndovu ambaye mbali na kuwa na uwezo huu hana utu au hisia kwa mnyama yeyote.

### 3.2.11 Zindukani

Mshairi hajatumia taashira kwa njia kuu katika shairi hili. Ametumia moja tu ambayo ni neno ‘ngoma’ ambalo ni ishara ya “raha” na “kucheza ngoma” ni ishara ya “kuponda na kufurahia” raha hizi.

### 3.3.0 TASHBIHA

Tamathali hii ya semi imetumika katika mashairi mengi ambayo tumechagua ili kutekeleza majukumu tuliyoshughulikia hapo awali katika sura ya pili. Mashairi haya ni kama yalivyo hapa chini.

### 3.3.1 N'shishiyelo ni lilo

Katika ubeti huu wa tisa, mshairi ametumia tashbiha. Aanasema:

> Kweli menifunga ndani,  ya chumba nde sitoki
>
> Kutwa kucha ni chumbani, juwa kuota ni dhiki
>
> Na mlinzi mlangoni, yu papo kattu ha'ndoki
>
> Nilindwavyo bilhaki, ni kama simba marara.

Tashbiha katika ubeti huu ni "ni kama samba marara".

Hapa, mshairi analinganisha kule kulindwa kwake na kule kwa simba marara. Huyu ni mnyama ambaye ni mkali mno ambaye kama yeye mwandishi hawezi kuachiliwa au kuwa huru kwa sababu atadhuru watu. Pia mwandishi amelinganishwa na "simba marara" kwa vile ni  mkali hata wakati amefungiwa chumbani lazima alindwe asije akatoroka. Akitoka huleta hasara kuu.

Katika ulingo wa siasa, msanii na chama chake walikuwa tisho kwa chama cha KANU; hasa yeye kwa kazi aliyoifanya ya kusambaza maoni yao miongoni mwa wananchi ambao wangekosa imani na serikali ya KANU.

### 3.3.2  Jipu

Mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa tatu mshororo wanne. Anasema:

Nna jipu lintunza, linipalo tabu mno

Tangu liliponianza, kamwe sipati usono

Kwamba ni mara ya kwanza,kuuguwa ndwezi hino

Latoma kama sindano, utunguwe nakwambiya

“Latoma kama sindano” ina maana kuwa lile jipu lina uchungu mwingi mno hivi kwamba mwandishi ahisi ni kama anachomwa mwilini vile sindano inavyomdunga mtu. Kutokana na uchungu huu msanii amekonda sana yaani hali yake ya mwili imedhoofika hivi kwamba “amekonda na kuwa kama uzi”. Mshairi ametumia tashbiha hii katika mshororo wa tatu wa ubeti wanne.

Nnakonda kama uzi, kwa kushitadi uchungu

Katika ubeti wa saba ametumia tashbiha nyingine akionyesha jinsi atakavyofanya mambo jipu likiiva. Asema:

Itimupo ndimi nalo, ja mwewe na mwana kuku.

Hapa mwandishi anaoyesha kasi au haraka atakayokuwa nayo kulifanya jipu limwishe mwilini yaani akipata nafasi ya kukata pingu au kufika mwisho wa kifungo chake ataipokea nafasi hiyo kwa haraka sawa na vile mwewe humchukua kifaranga kabla atambue hila za mwewe na kutoroka.

Tashbiha nyingine imetumika ubeti wa tisa. Mshairi asema ataliminya jipu lisimsumbue tena hadi “midamu itiririke kama ng’ombe alonona” yaani atapambana na dhuluma zote kisiasa na

kuwa huru. Hizi dhuluma zitatoka kwa njia ya kupigana hadi damu itiririke kama vile inavyofanyika ng'ombe mnono akichinjwa. Huku kupigana ndiko kuliminya litumbuke kama mshairi anavyosema katika ubeti huu mshororo wa kwanza.

Taliminya litumbuke, lisinisumbue tena
Usaha wote utoke , utoke nikiuona
Midamu itiririke, kama ng'ombe alonona.
Jipu hili mwana lana, M'ngu mbwalipa hizaya.

### 3.3.3 Siwati

Katika shairi hili, mshairi azungumzia kutoacha imani yake. Ametumia tashbiha katika kulinganisha watu wale wanaoacha imani na nzi. Nzi ni mdudu mchafu ambaye hatulii bali huruka huku na kule, akitua hapa na pale akigusa hiki na kile, akila chochote yaani nzi hana msimamo. Hivyo mwandishi hawezi kuacha imani yake akakosa kuwa na msimamo. Asema katika ubeti wa nne:

Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi
Siwati ningaambiwa, niaminiyo hayawi
Siwati kisha nikawa, kama nzi, hivyo siwi
Thamma nakariri siwi, na M'ngu nisaidiya

### 3.3.4 Mamba

Mwandishi azungumzia kiongozi ambaye ajigamba kuwa ataishi milele. Huyu ni kiongozi wa kiimla. Mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa kwanza anaposema, anataka kusema na

kusema kwake kulinganishwe na kwa wale wasemao yaani kama kwa viongozi. Hili neno wambao pia linalinganishwa na watu wenye ujuzi. Mshairi asema:

‘Nami nambe, niwe kama waambao’

### 3.3.5 Mnazi: Vuta N’kuvute

Shairi hili lazungumzia mvutano baina ya kiongozi ambaye amewadhulumu wananchi. Kiongozi anawakilishwa na BADI na ALLI anawakilisha wananchi ambao wamenyimwa haki. Msanii ametumia mbinu ya tashibiha katika ubeti wa ishirini na saba. Mshairi asema:

Fungu ulo ukinipa, wakati unapogawa
Sababu iliyonipa, hakataa kutukuwa
Ulikuwa ukinipa, ukinipa kama dawa
Hali tuna haki sawa

Tashbiha “ukinipa kama dawa” inatumika kurejelea matunda yaliyotokana na maendeleo ya nchi viongozi waliwagaia wananchi kwa kiasi kidogo sana kinawafikia hivi kwamba hakitoshi. Kiasi chatolewa kama dawa. Dawa hutumiwa si kwa hiari ya mtu bali kutokana na maelezo ya daktari yaani kiasi cha dawa ni hiari ya mwingine, hiari yake BADI. Pia hazimezwi kwa wingi, ni kidogo.

Mwandishi ametumia tashbiha nyingine katika ubeti wa thelathini na tano. Asema:

‘Wewe ni mbubukwaji, maneno mengi kanwani
Ambaye ni mtendaji, alilonalo haneni
Hutuliya kama maji, yaliyomo mtungini
Kangoja siku ya zani

Mshairi asema kupitia BADI akimwambia mwenzake ALII hastahili cheo chake kama ni mtendaji angetulia kama maji ya mtungi. Tashbiha hii inalinganisha utulivu na ule wa maji ya mtungi. Maji huwa hayafanyi kelele yoyote yakiwa mtungini.

Katika ubeti thelathini na sita, mwandishi ametumia tashbiha nyingine ambayo ni:

Henendi kumuoteya, ja kifaranga na mwewe

Mshairi amaanisha kwamba shujaa hajitokezi akiwa kama kwamba ajificha kama vile mwewe anavyomvizia kifaranga na kujitokeza ghafla na kumchukua bila ya yeye kutarajia.

### 3.3.6 Telezi

Katika shairi hili, mshairi azungumzia ukoloni mamboleo ambao uliendelezwa na viongozi ukazua matatizo katika nchi hivi kwamba maendeleo yaliyokuwa yametokea hayakunufaisha wananchi. Licha ya matatizo haya mshairi akaamua kung'ang'ania haki japo kwa dhiki. Haya asema katika ubeti wa sita lakini hakujua alikuwa ni "mfano wa samaki kwendea ndoana". Hii ni tashbiha yenye maana kuwa samaki aonapo chambo hukiendea ili kimnufaishe kama chakula lakini punde amezapo huwa amenaswa na kujikuta katekwa na mvuvi akafanywa kitoweo. Hivi ndivyo mshairi alivyojaribu kuyafikia maendeleo ya nchi anufaike kwayo ingawa kwa kupigania lakini akashikwa na ndoana ya mvuvi (wapinzani wake kisiasa) na kubwagwa na utelezi. Yaani aliishia kizuizini.

### 3.3.7 Semeni Wenye Kusema

Katika shairi hili, mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa kwanza.Anasema katika mshororo huu:

> Mbona leo hamusemi, mu kimya kama mapumbe

Anawaambia wasemaji, waseme waache kuwa kimya kama kwamba wao ni wajinga. Mshairi anamaanisha wajinga ndiyo hunyamaza pengine kwa kuwa hawana la kusema . Maadamu hawa anaozungumzia ni wenye kusema na hawasemi, mshairi alinganisha vinywa vyao na vile vya wapumbavu.

Tashbiha nyingine imetumika katika ubeti wa pili; mshairi asema:

> Ni mawi yaliyotuka,' ni ya ki utu' musambe
> Ni yupi mwenye kutaka, kama hayo yamkumbe
> Hao yaliyowafika, ni kama 'mefumwa chembe
> Msijifanye migombe, semeni wenye kusema.

Mshairi alitumia tashbiha kuwa wale wamepata mambo mabaya wakawa kama waliyopigwa mshale (ni kama 'mefumwa chembe). Huku kupigwa chembe ni sawa na kujeruhiwa usiweze kupigana. Hawa ni wale waliyohasirika kisiasa. Mtu akipigwa mshale huenda akafa au akinusurika huwa mlemavu kwa majeraha. Hivyo kufuma chembe ni sawa na kuhasirika kisiasa.

### 3.3.8 Muwerevu Hajinyowi

Mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa kwanza asemapo:

Mwenye nacho wajishasha, wajiona kama ndovu

Mshairi alinganisha nguvu za wenye mali na zile za mnyama ndovu ambaye kati ya wanyama wengine yeye huwa na nguvu kushida mnyama mwingine yeyote.

### 3.3.9 Mambo Yana Mambo Yake

Katika shairi hili mshairi anazungumzia kuhusu mambo anayosema yanahitaji ujuzi. Katika ubeti wa kumi ametumia tashbiha kulinganisha jinsi matatizo hutokea na kutanda kama matandu yanavyotanda. Mshairi asema:

Mambo yataka ujuzi, kijinga hayatakwenda
Yataka mtu maizi, mjuzi kuyatenda
Zitatanapo tatizi, Kama matandu kutanda.
Ziwe hazitamshinda, kuyatatuliya mambo

Matatizo "yakitanda kama vile matandu hutanda" huwa ni sawa na matatizo kuwa yamefichamana na kufunikwa hivi kwamba kuyatatua ni vigumu na kunahitaji mtu mwenye ujuzi ili asishindwe.

Mwandishi ametumia tashbiha nyingine katika ubeti wa ishirini na nane. Mshairi asema katika ubeti huu:

Yataka imani kweli, tena ilotimilika

Thabiti kama jabali, isoweza kuondoka

Ikumbwako na kitali,siwe nda kutikisika

Ile vyema kutendeka, yataka imani mambo.

Jabali kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2004 :166) ni mwamba mkubwa au kilima au mlima wa mwamba. Katika ubeti wa ishirini na nane mshairi analinganisha kuwa imara kwa imani na vile mwamba unavyokuwa thabiti hivi kwamba hautikisiki hata ukipigwa na dhoruba inakuwa vigumu. Mtu mwenye imani thabiti yaani iliyo imara kama jabali ndiye ayaweza mambo. Imani yaendelea kulinganishwa na mama katika ubeti wa thelathini mshairi anaposema:

Mambo yaendapo popote, imani isiwe nyuma

Yendapo yenende wote, ndio mambo yawe mema

Katika mambo yoyote, imani ni kama mama.

Mama ni mwanamke ambaye humzaa mwana na kumlea kwa kumpa chakula, kumyonyesha na kumkinga. Hutambua wakati mwana ni mgonjwa na kumshughulikia vilivyo. Yaani mama ni kiumbe ambaye binadamu hutegemea kwa njia kuu akiwa mchanga na akiwa mzima kwani alivyofunzwa akiwa mdogo humwandama utu uzimani. Imani imelinganishwa na mama kwani ili mambo yatendeke vyema binadamu ahitaji kuwa na imani popote pale na daima. Bila mama mtoto hawezi kuzaliwa au kuonekana duniani. Vivyo hivyo imani ni chanzo cha mambo yote kwa binadamu kama vile mama ni chanzo cha yote kwa mtoto.

### 3.3.10 Jana na Leo na Kesho

Mwandishi ametumia tashbiha katika ubeti wa ishirini asemapo:

> Kesho mithili ya mwana, aliyemo matumboni
>
> Hujui ni mvulana,msichana au nani
>
> Au kama atapona,ajapo ulimenguni
>
> Huwa hunayo yakini

Kesho imelinganishwa na kilinge ambacho hakijazaliwa hivyo hakijulikani kama kitakuwa mvulana au msichana au kitakuwa kizima au kitakufa.

### 3.3.11 Usiniuwe

Mshairi ametumia mbinu ya tashbiha katika shairi hili lenye maombi mengi ya mwana ambaye hajazaliwa kwa mzazi ili asimwue. Mwana katika ubeti wa kumi na tatu anamwambia mama:

> Usiwe sawa na nduli, mamangu nihurumiya

Mshairi ametumia tashbiha ya kulinganisha mama na nduli. Yaani mama asiwe shetani au katili kwa mwanawe akamuua.

### 3.3.12 Ndiya Panda

Anwani ya shairi hili ina maana ya kutatiza. Mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa kumi na nne. Anasema:

Ni kama niloangama, na kushuka kwanishinda
Na hata lau nasema, nijitupe kama bunda
Sitaanguka salama, kwenye mawe ‘tajidunda

Katika mshororo wa kwanza mshairi anajilinganisha na mtu aliyekaa katika sehemu ya juu na anashindwa kuteremka. Asema hata kama angejitupa kama mzigo yaani kujiangusha kwa nguvu ajua hataanguka salama kwa vile hali (mawe) ni ngumu. Mshairi alinganisha kujitupa kwake na kule kuangushwa kwa mzigo. Hata akifanya hivi, anasema hatashinda (sitaanguka salama) vita.

### 3.3.13 Kichu Hakiwi ni Uchu

Mshairi aeleza kuwa hakuna kitu chochote ambacho chaweza kuwa utu. Anatumia tamathali ya semi tashbiha, anapoyanena haya. Katika ubeti wa kumi na tano asema:

Changu ni cha Kimvita, tangu mwa mama tumboni
Sikwenda kukitafuta, nlikikuta nyumbani
Mi nacho kama pata, twendapo hatuwatani

Tashbiha ni “mi nacho ni kama pata”.Mshairi hapa alinganisha lugha yake na hali ambayo mtu hujipata nayo ambayo hawezi kuibadilisha; ni sehemu ya binadamu mwenyewe.

Katika ubeti wa kumi na saba mshairi asema Kiswahili kwake ni “kama asali”. Analinganisha Kiswahili na asali. Asali ni tamu mno na utamu huo haukinaishi. Hivyo Kiswahii ni lugha nzuri. Tashbiha nyingine imo ubeti wa ishirini na tisa. Mshairi asema binadamu ambaye huwa na mali nyingi kama milima ila hamfai binadamu mwenzake huwa “sawa na mnyama”. Huyu binadamu amelinganishwa na mnyama kitabia kwa kukosa hisia za utu.

Mshairi  katika ubeti wa thelathini na nane asema:

Ndovu na bakhili sawa, hawa mbali kwa masafa

Ndovu ni mnyama mwenye nguvu na uwezo mkubwa. Hakuna chochote cha ndovu kinachotumiwa akiwa hai lakini afapo binadamu hufaidi kwa pembe na nyama yake. Huyu ndovu ni kiongozi mwenye uwezo mkuu ambaye hawezi kuachilia uongozi umwendee mwingine, ni kifo tu kitawapa wengine nafasi ya kuchukua uongozi huu. Hivyo mshairi amemlinganisha  kiongozi na bakhili ambaye ni mchoyo.

### 3.3.14  Zindukani

Mshairi ametumia tashbiha katika ubeti wa tatu. Anasema:

U-Badi mewapoteza, mukakosa kuelewa

Ndiwo ulowamaliza, leo mu kama mabuwa

"Leo mu kama mabuwa" ni tashbiha ambayo inalinganisha watu fulani ambao walikuwa na thamani lakini sasa hawana tena.Thamani yao ni ndogo. Ni mabua  ambayo  yakiwa katika hali hii hayana faida yenye maana kwa yeyote.

### 3.3.15  Hitimisho

Katika sura hii ya tatu, tumeshughulikia tamathali za semi za istiari, taashira na tashbiha  katika mashairi teule kutoka diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Si mashairi yote tuliyochagua yana mbinu hizi zote tatu.  Mshairi yetu yote yametumia istiari isipokuwa shairi "Siwati". Nusu ya mashairi haya yametumia taashira na kumi na manne yametumia tashbiha.

Katika sura itakayofuata tumeshughulikia majukumu ya istiari, tashbiha na taashira katika uwasilishaji wa dhamira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*.

# SURA YA NNE

## 4.0 Majukumu ya Istiara, Tashbiha na Taashira katika Uwasihishaji wa Dhamira Katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki.*

Hapa tutashughulikia majukumu ya mbinu hizi tatu za ulinganishi kufikia dhamira ya mwandishi katika *Sauti ya Dhiki.*

## 4.1 Utangulizi

Kama vile mshairi huwa na dhamira fulani anapoandika mashairi yake kwa jamii,vivyo ndivyo ilivyo kwa mbinu anazotumia . Kila mbinu hubeba majukumu yake katika kufikia dhamira ya mwandishi. Hata hivyo kuna majukumu ya kijumla ambayo ni ya kuhamisha maana kama asemavyo Leech (1969) kwamba sifa za ‘F’ zinaweza kuchukuliwa na ‘L’ ikiwa “F” ina uhusiano na “L” kwa njia moja au nyingine. Majukumu haya yameshughulikiwa hapa chini.

## 4.2 Majukumu na Dhamira

Kila matini huwa na majukumu na dhamira kwa jamii lengwa ambayo mshairi hunuia yafikie jamii hii. Diwani ya S*auti ya Dhiki* ina majukumu na dhamira ambayo yamefumbatwa katika tamathali za semi ambazo ni istiari, tashbiha na taashira kati ya zingine ambazo hatukushughulikia. Tamathali hizi tatu zimechochea fikra za msomaji ili aweze kupata ujumbe kwa undani na hivyo kufikiwa na dhamira ya mwandishi ya kuwasilisha kilio cha mshairi kwa hadhira ambayo ni wananchi waliokuwa na maoni sawa naye ya kisiasa. Pia kwa wengine ambao wangepata kilio chake na kujiunga naye katika mapigano ya kisiasa.

Abdilatif alidhamiria kuficha ujumbe wake, ili ufikie hadhira yake teule. Hivyo, akatumia mbinu za istiari, tashbiha na taashira ili kusimamia mambo ya kisiasa ambayo hangetaka yagunduliwe moja kwa moja. Hili lilichochewa na hali ya kisiasa ya wakati wake kwani angedhulumiwa zaidi kama ujumbe wake ungekuwa wazi. Hili lathibitishwa na Chacha (1992) asemapo mbinu hizi hutumika kuficha habari aliyokusudia ili isiwafikie watu ambao wanadhaniwa wanaweza kumwangamiza mshairi. Kwa mfano katika mashairi “Usinuwe”, “Mnazi” na “Jipu”.
Mwandishi ameweza kufikia dhamira ya kuficha ujumbe, kwani yeyote ambaye hakujua historia yake na ya siasa za nchi wakati wake, hangetambua kuwa mashairi yanazungumzia maswala ya kisiasa bali mambo ya kawaida tu katika jamii.

Jukumu lingine la matumizi ya istiari, tashbiha na taashira katika kutekeleza dhamira ni kuleta au kujenga mshikamano wa kisemantiki katika kazi ya kifasihi. Wamitila (2008) asema mshikamano wa kisemantiki unaweza kuimarishwa kwa unasibishi na uhusishi wa ishara zilizotumiwa katika matini. Abdilatif ameimarisha muala na ujenzi wa kisemantiki kwa kutumia mbinu hizi tatu kati ya zingine pamoja na mifanyiko ya kisintaksia ambayo inahusisha ubadilishanaji wa aina za maneno kwa mfano kiwakilishi huchukua mahali pa nomino. Hili limetokea, kwa mfano, katika shairi “La Mjini na La Shamba”. “La” ni kiwakilishi cha nomino “jogoo” ambayo ni istiari.

Tamathali hizi huleta mshikamano wa kisemantiki kwa udondoshi. Kwa mfano, kwa kutumia ishara kama bendera, safari, msitu, mama na ndiya panda katika baadhi ya mashairi tuliyoshughulikia katika sura ya tatu, mshairi amedondosha maelezo mengi mno. Kwa mfano neno “bendera” linaweza kuwa na maelezo ya kujitawala, uhuru, kujiendeleza kwa nchi bila

pingamizi pia kuwa washindi. Vile vile neno “mama” limesheheni maelezo kama mzazi wa kike, mfariji na mwalimu maishani. Mshairi anapotumia udondoshi anatumia lugha ya mkatomkato. Chimera na Njogu (1999) wanakubaliana na jambo hili wasemapo kuwa lugha ya ushairi ni tofauti na ya kawaida kwa sababu maelezo yake ni ya mkatomkato. Hivyo, inamjuzu mhakiki aitafakari lugha sio tu kama chombo cha fasihi, bali pia kama chombo kinachosheheni maana.

Mshairi wa diwani ya *Sauti ya Dhiki* alinuia kuboresha kazi yake. Hili ni jukumu lingine la istiari, tashbiha na taashira. Uboreshaji huu unahusu kujenga na kufanikisha ucheshi kulingana na hulka ambazo huzua hisia tofauti tofauti kwa mfano mshairi amezua ucheshi anaporejelea wazo kama manii tone moja la maji madhalilifu au kurejelea viongozi kwa maneno kama ndovu, mamba, ndugu ulo mnazini, simba na kadhalika. Ucheshi huu umezua burudani ambayo humfanya msomaji afurahie mashairi haya anapoyasoma na kuhakiki mbinu hizi za istiari, tashbiha na taashira.

Tamathali hizi za istiari, tashbiha na taashira zimetumika na mshairi ili kuleta tasfida. Tasfida hii imesaidia mwandishi kuepukana na utovu wa nidhamu katika matumizi ya lugha. Pia ameepukana na kuzua hisia hasi wakati wa kushambulia maovu katika jamii. Kwa mfano anaposhambulia viongozi ambao wamewanyima haki wananchi na kujiona ni wenye uwezo mkuu na wakamilifu kwa kila njia. Hili lawafanya kuwatawala wananchi na kuwatendea maovu bila huruma.Hivyo wamekashifiwa wasiwatawale wananchi bila huruma hadi wasijue la kufanya kama mshairi asemavyo kwa kutumia taashira njia panda. Istiari, tashbiha na taashira ni tamathali ambazo mshairi ametumia kufikia dhamira yake ya kuzua tashititi.Tashtiti kama

asemavyo Mbatia (2001) ni kunga ya utunzi inayoshambulia maovu ya jamii na dosari za kitabia kama vile uzandiki kwa kubeza au kudhihaki. Mbinu hii ya tashtiti hutumiwa kumulika matendo ya wahusika na hali fulani, ili kuzikashifu hali hizi, matendo na matukio. Mshairi katika diwani ya S*auti ya Dhiki* ametumia tamathali za istiari, tashbiha na taashira kudhihaki wahusika ambao ni viongozi katika mengi ya mashairi yake, pia hali mbaya za ukandamizaji wa wananchi waliowakashifu wanasiasa na kuwambia ukweli. Kwa mfano, baada ya mshairi kuwakabili wanasiasa na ukweli alitiwa kizuizini. Amekashifu jinsi maisha ya kizuizini yalivyo kwa mfano, atumia tashbiha hii kuwa alindwa kama simba marara hata baada ya kuwa katika kuta ndefu. Pia akashifu matendo ya viongozi ya kujitwalia mali katika shairi "Mnazi: Vuta N'kuvute" na "Telezi" kwa kutumia tamathali taashira kama tope na mijaji kwa mikondo barabarani ambazo ni dalili za maendeleo ambayo hayakufikia wananchi. Pia katika shairi "Jipu" ambapo matendo ya viongozi kwa mshairi ni kama jipu lenye uchungu usio mithilika. Katika shairi "kichu Hakiwi ni uchu" awanarejelea viongozi kama wanyama wa pori.

Jukumu lingine la tamathali hizi za istiari, tashbiha na taashira ni kumsaidia mshairi kufikia uumbaji wa mashairi. Hii ni dhamira kuu ambayo ameifikia. Mbinu hizi hutumika kama njia ya kumpatia misamiati ambayo imeunda mashairi. kwa kutumia vilinganishi kama ndovu, simba, mamba na pweza, mshairi amepata maudhui ambayo yanarejelewa na sifa za wanyama hawa kwa wahusika wa mashairi yake na kuzua hisia kwa wasomaji. Mbinu hizi pia huleta uhondo katika uumbuji wa mashairi.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia majukumu ya istiari, tashbiha na taashira ambayo amefanikisha kufikia dhamira ya mwandishi katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Majukumu haya ni urembeshaji wa kazi, kuficha ujumbe kuleta tasfida kufanikisha uumbaji wa mashairi na kuleta mshikamano wa kisemantiki.

Sura ya tano tutashughulikia hitimisho la utafiti wetu ambalo linahusu ujumlishaji wa tuliyoshughulikia ambayo ni uthibitishaji wa madhumuni, upimaji wa nadharia tete na mapendekezo.

# SURA YA TANO

## 5.0 Hitimisho na Mapendekezo

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia hitimisho la utafiti wetu na kuthibitisha makisio au haipothesia zetu na mwishowe kutoa mapendekezo kwa watafiti wengine.

### 5.1.0 Hitimisho

Katika tasnifu hii tumechunguza matumizi ya istiari, tashbiha na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Tulitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo na kuangazia mambo ya kimsingi ambayo hushughulikiwa katika kazi ya kifasihi inapotumia nadharia hii. Tumeshughulikia matumizi ya mbinu hizi kwa jumla na vile vile katika kazi mbalimbali na mwishowe tukashughulikia yaliyosemwa kuhusu diwani ya *Sauti ya Dhiki*.

Katika sura ya pili tumeangazia mbinu za istiari, tashbiha na taashira. Kisha tukaonyesha mbinu hizi kutoka mashairi teule ya diwani ya *sauti ya Dhiki* katika sura ya tatu. Baadaye tukashughulikia majukumu ya mbinu hizi ili kufikia dhamira ya mwandishi.

Tulizingatia tamathali za semi istiari, tashbiha na taashira kama zilivyotumika katika diwani ya S*auti ya Dhiki* kwa kutumia sampuli ya kusudi na kuchagua mashairi ishirini. Utafiti wetu umeonyesha uhusiano wa karibu wa tamathali hizi tatu kwa kuwa kimsingi ni mbinu za ulinganishaji. Kutokana na mbinu hizi za istiari, tashbiha na taashira, mashairi ya Abdilatif yametia fora katika kuonyesha hali ya juu ya kutumia kilicho cha kawaida katika jamii kueleza kisicho cha moja kwa moja katika jamii.

### 5.1.1 Madhumuni ya utafiti

Katika kazi hii tulinuia kufanya mambo mawili. Kwanza tulinuia kuonyesha taashira, istiari na tashbiha zilizotumika katika *Sauti ya Dhiki.* Tumelionyesha hili katika sura ya tatu. Tumeonyesha na kufafanua matumizi ya tamathali hizi tatu katika mashairi teule kama zilivyojitokeza. Pili, tumetathimini mchango wa tamathali hizi katika kuwasilisha dhamira katika diwani *Sauti ya Dhiki*. Haya tumeyashughulikia katika sura ya nne ambapo tumejadili majukumu na dhamira za mwandishi. Nazo ni kuboresha kazi, kutoa ujumbe kwa njia fiche, kujenga mshikamano wa kisemantiki, kuleta tasfida na kufikia uumbaji wa mashairi.

### 5.1.2 Matokeo kuhusu nadharia tete

Abdilatif ametumia tamathali za semi, istiari, tashbiha na taashira katika mashairi yake. Sio kila shairi limetumia mbinu hizi kwa wakati mmoja lakini zote zimetumika kwa ukwasi wa hali ya juu. Mbinu hizi zimetumika kama mihimili ya maudhui mengi ya mashairi haya kwa wasomaji au walengwa. Hivyo nadharia tete zetu ambazo ni kuwa mtunzi wa diwani ya *Sauti ya Dhiki* ametumia mbinu ya istiari, taashira na tashbiha ni kweli. Pia makisio yetu kuwa tamathali hizi zimetumiwa kwa mwelekeo mwema na wa kufana kuwasilisha dhamira yake yamethibitika.

## 5.2 Mapendekezo

Kila mhakiki ana uelewa tofauti na mwingine, hivyo ningewaomba wahakiki wengine washughulikie mbinu hizi pamoja na nyingine nyingi alizotumia Abdilatif kuonyesha uhondo na uboreshaji wa kazi za kifasihi. Jambo hili huenda likachochea wengine kuandika mashairi na uhakiki kuendelea.

Pia kulingana na upeo na mipaka yetu hatukushughulikia mashairi yote ili kuonyesha tamathali hizi za istiari, tashbiha na taashira. Hivyo twapendekeza wahakiki wengine wafanyie utafiti tamathali hizi tatu katika mashairi mengine yaliyosalia. Pia wanaweza kuangazia sehemu kama sarufi na mtindo, muala na mshikano na kutumia nadharia zingine kama uhamisho na ya upole katika uhakiki zaidi wa mbinu za uandishi.

## MAREJELEO


Abed, K.A (1954) *Sheri za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amir*. E.A. Publishing House Dar es Salaam.

Abdilatif, A. (1973) *Sauti ya Dhiki* Oxford University Press. New York.

Abdulaziz, M. H (1979) *Muyaka 19th Century Kiswahili Popular Poetry*. Kenya Literature Bureau. Nairobi.

Abraham, M.H (1941) *Glossary of Literary Terms*. 3rd Ed. New York. Holt, Reinhert Winston Inc.

Abraham,M.H (1957) *Glossary of Literary Terms.7th Ed*. New York.Holt Reinhert Winston Inc.

Arege, T. (2012) *Narration in Swahili Narrative Poetry. An Analysis of Utenzi wa Rasi Ighuli.* Shahada ya Uzamifu. Haijachapishwa.

Barry, P. (2002) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. 2nd Ed. Manchester University Press U .S.A.

Chacha, N. Chacha (1980) *Ushairi wa Abdilatif Abdalla. Tasnifu ya Uzamili.* Haijachapishwa. U.O.N.

________________ (1992) *Ushairi wa Abdilatif Sauti ya Utetezi.* Dar es Salaam University Press. Dar es Salaam.

Coward, David (2002) *A History of French Literature from Chanson De Geste to Cinema.* Blackwell Publishing Ltd U.S.A.

Day-Lewis, C. (1947) *The Poetic Image.* The City of Oxfords. Britain.

Fiumara, G.C (1995) *The Metaphoric Process; Connections Between Language and Life.* Routledge. London.

Harries, Lyndon (1962) *Swahili Poetry.* Oxford University Press. London.

Kineene wa Mutiso (2005) *Utenzi wa Hamziyya TUKI*. Dar Es Salaam.

Kithaka wa Mberia (2001) *Bara Jingine* Marimba Publications. Nairobi.

Knappert, J. (1992) *Utenzi wa Kalevala*.TUKI.Dar es Salaam.

Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Semi.* E.A Literature Bureu, Dar es Salaam

Leech, G.M (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. Longman England.

Leech, G.M na Short, M. (1981) *Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose*. Longman London.

Lugwiri, P.L. (2011) *Sitiari, Taashira na Tashbiha Katika Uwasilishaji wa Dhamira Katika Utenzi wa Taambuka*. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa .U.O.N.

Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Standard Text Books Graphics and Publishers. Nairobi.

Mlacha, A. na Hurskainen, A (1995) *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. TUKI. Dar es Salaam.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Kifasihi.* East African Education Publishers. Dar es Salaam.

Muasya, J.N (1991) *Maudhui Katika Sauti ya Dhiki*: Tasnifu ya Shahada ya Ualimu. Haijachapishwa.

Mohamed, S.A (1995) *Kunga za Natharia ya Kiswahili*. *Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. E.A Educational Publishers. Nairobi.

Mwangi, R.J (1992) *Suala la Siasa Katika Sauti ya Dhiki*. Tasnifu ya Shahada ya Elimu. Haijachapishwa. UoN.

Myers, T. And Simms, M. (1989) *The Longman Dictionary of Poetic Terms Longman.* London.

Nabukonde, L. L. (2011) *Symbolism in Uganda Poetry*. Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapisha. U.O.N.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*, Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Northrop Fyre na Wengine (1985) *The, Harpes Handbook of Literature.* New York. Harpes and Row.

Timammy, R. (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs.* A Stylistic Analysis. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Haijachapishwa, U.O.N.

Simpson, P. (2004) *Stylistic*: *A Resource Book for Students*. Routledge London.

Thrall,W. na Hibberd, P. (1960) *A Handbook of Literature.* Odssey Pres New York.

TUKI (2004) *Kamusi Sanifu ya Kiswahili.* Sanifu Oxford University Press East Africa Ltd. Kenya.

Wales, K. (2001) *A Dictionary of Stylistic*. Pearson Education Limited. Harlow Eng.

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi*, Vibe-Muwa Publishers Ltd. Nairobi.

Wamitila, K.W (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Focus Publishers:Nairobi.

__________________ (2008) *Kanzi ya Fasihi: Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*. Focus Publishers: Nairobi.

William, H. (2003) *A Hand Book to Literature.* 9th Edition. Prentice Hall: Upper Saddle River. New Jersey